**Rais** Samia aonya hujuma dhidi ya ndege za serikali

UKURASA 2



**Mrithi** wa Mfugale TANROADS ateuliwa, Profesa Mgaya aula

UKURASA 3




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Julai 31, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580658

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Vituo 550 vya chanjo corona

## MASHARTI manne yawekwa, wananchi waweka kando tahadhari... *Endelea ukurasa 2*




Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa pamoja na viongozi mbalimbali akikata utepe kuashiria kupokea ndege mpya aina ya Bombadier DASH 8-Q400 iliyonunuliwa na Serikali ya Tanzania na kukodishwa kwa Shirika la Ndege la ATCL, ilipowasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana. Wa pili kushoto ni Makamu wa Rais, Dk. Philip Isdor Mpango na wa tatu kulia ni Waziri Mkuu Kassim Majaliwa. **PICHA: IKULU**

## Kamati kuadhibu wakiuka maadili

UKURASA 5



## Korti yatupa ombi la utetezi kesi ya Sabaya

UKURASA 2

**MICHEZO** POLISI TANZANIA FC, BABA YAKE MDAMU WAFUNGUKA UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Korti yatupilia mbali ombi la utetezi kesi ya Sabaya

**Na Allan Isack, ARUSHA**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, imetupilia mbali ombi dogo la mawakili wa utetezi katika kesi ya aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya la kutaka maelezo ya awali yaliyoandikwa katika Kituo Kikuu cha Polisi cha Arusha.

Maelezo hayo ni yale yaliyoandikwa na shahidi wa sita wa Jamhuri katika kesi hiyo, Bakari Msangi (38). Mawakili hao waliomba maelezo hayo yatumike kama sehemu ya kielelezo cha ushahidi kwa kuwa utaratibu wa uwasilishwaji ulikosewa.

Mbali na Sabaya, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Sylvester Nyegu (26) na Daniel Mbura wanaokabiliwa na mashtaka matatu ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Akitoa uamuzi huo mdogo, Hakimu Mkazi Mwandamizi Odira Amworo, alitupilia mbali ombi hilo kutokana na sababu mbalimbali baada ya la Mawakili wa Utetezi kutumika kama sehemu ya kielelezo cha ushahidi katika kesi hiyo.

"Baada ya kusoma uamuzi wa pande zote mbili, mahakama ilirejea kwenye baadhi ya kesi katika Mahakama ya Rufani na ilainisha utaratibu wa kufuata moja maelezo ya shahidi yanatakiwa kusomwa, alisema Hakimu Mkazi Odira Amworo wakati akitoa uamuzi huo.

"Pili shahidi lazima arejeshwe kwenye maeneo la ushahidi wake ambao unatakiwa kutikiswa na tatu lazima nyaraka itolewe kama ushahidi mahakamani. Katika hatua ya kwanza haikutekelezwa, hivyo mahakama imekubali kuwa pingamizi limekubaliwa," aliongeza.

Juzi wakati mawakili wa utetezi wakimhoji shahidi huyo wakiongozwa na Wakili Moses Mahuna, waliiomba mahakama watumie kielelezo cha maelezo ya awali ya shahidi huyo kama sehemu ya ushahidi mahakamani.

Baada ya ombi kutolewa, kulitokea mabishano makali ya kisheria kati ya upande wa Jamhuri na wa utetezi.

Mawakili wa Jamhuri wakiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu Tuamini Kweka, Wakili wa Serikali Mwandamizi Abdalah Chavula na Wakili wa Serikali Baraka Mgaya, walipinga ombi la utetezi kwa madai kuwa hawakufuata utaratibu wa kisheria na wa kimahakama.

Wakili Chavula alidai mahakamani hapo kwamba kuna utaratibu wa kuwasilisha ombi hilo ambao haukufuatwa, hivyo kuiomba mahakama kutupilia mbali ombi hilo.

"Mheshimiwa Hakimu kwa kuwa ndugu zetu wa utetezi hawakufuata kanuni na utaratibu wa kimahakama kuomba nyaraka hii kutumika kama sehemu ya ushahidi, tunaomba mahakama yako tukufu itupilie mbali ombi lao,"alidai Chavula.

Mbali na mawakili wa Jamhuri kuiomba mahakama hiyo kukataa nyaraka ya maelezo hayo kutumika kama sehemu ya ushahidi, pia shahidi naye aliiomba mahakama hiyo kutumia ushahidi alioutoa mahakamani badala ya maelekezo alioandikisha kituo cha polisi Februari 9 na 16, mwaka huu.



Mwenyekiti wa Kamati ya Amani ya Viongozi wa Dini Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, baada ya kuchaguliwa tena kuwa Mwenyekiti mpya wa kamati hiyo juzi. Katikati ni Katibu Mkuu wa kamati hiyo, Askofu Israel Maasa na Naibu Katibu Mkuu, Sheikh Dk. Amri Juma. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Vituo 550 chanjo corona

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI huduma ya chanjo ya UVIKO-19 ikitarajia kuanza kutolewa kwa wananchi kuanzia Jumanne ya wiki ijayo kwenye vituo 550 katika mikoa ya Tanzania Bara, serikali imetoa masharti manne ya kuchanja.

Katika taarifa iliyotolewa jana jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Abel Makubi, vituo takribani 550 vitatumika kutoa huduma hiyo.

Prof. Makubi alitaja masharti ya kupata chanjo hiyo ni pamoja na wanaotaka kuchanja, kutakiwa kujisali kwa kutumia mtandao wa ndani ya simu au kompyuta.

Alisema anayefanya 'booking' ya siku ya kuchanja anaweza pia kwenda kwenye kituo na kujisajili kuanzia Jumatatu ya wiki ijayo pamoja na kujaza fomu ya uhiari wa kuchanjwa.

Prof. Makubi alisema sharti lingine ni chanjo hiyo itaanza kutolewa kwa makundi yenye uhitaji mkubwa, ambayo ni watumishi wa sekta ya afya, watu wazima kuanzia umri wa miaka 50 na kuendelea na watu wenye magonjwa.

Alisema wananchi wanaotaka kwenda kuchanja, wanatakiwa kujihakiki kama wapo katika makundi hayo kabla ya kupokea chanjo.

"Kutokana na mwongozo wa chanjo wa taifa dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19, ule wa Shirika la Afya Duniani (WHO), maelekezo ya Covax Facility na upungufu wa uzalishaji wa chanjo toka viwandani, chanjo hizi kwa sasa zinatolewa kwa kufuata vipaumbele vya makundi yenye uhitaji mkubwa," alisema Prof. Makubi.

Aliendelea kufafanua: "Serikali inategemea kutoa chanjo kwa makundi yanayolengwa kuanzia Agosti 3, mwaka huu, siku ya Jumanne katika vituo 550 vya kutolea huduma katika mikoa yote ya Tanzania Bara."

Prof. Makubi alisema walengwa wanapaswa kwenda katika vituo hivyo wakiwa na kitambulisho cha kupigia kura au leseni ya udereva, hati ya kusafiria na kitambulisho cha uraia.

Alisema makundi mengine yataendelea kupata chanjo katika awamu zinazofuata mara zitakapowasili nchini.

Serikali ilipokea chanjo 1,058,400 ya UVIKO-19 aina ya Johnson & Johnson wiki iliyopita kutoka Serikali ya Marekani kupitia mpango wa Covax, unaolenga kusaidia nchi zinazoendelea katika kukabiliana na janga hilo.

Rais Samia Suluhu Hassan alizindua chanjo hiyo kitaifa kwa kuchanja Ikulu jijini Dar es Salaam.

**HADHARI KANDO**

Wakati serikali ikisisitiza ugonjwa huo unaendelea kuchukua maisha ya wananchi, mkoani Dar es Salaam, hadhari na miongozo ya kukabiliana na baa hilo ni kama imepuuzwa.

Nipashe ilishuhudia jana katika masoko (mfano Mwenge), usafiri wa daladala na treni, wananchi wakiwa wamesongamana bila kuchukua tahadhari yoyote ikiwamo kuvaa barakoa.

Kwenye usafiri wa mabasi yaendayo haraka, maarufu Mwendokasi, Nipashe ilishuhudia abiria wakiwa wamevaa barakoa wakati wa kukata tiketi, lakini baadhi yao walizivua walipoingia ndani ya mabasi huku ndani ya mabasi hayo kukiwa na msongamano mkubwa wa abiria.

"Siwezi kuvaa barakoa kwa kuwa mazingira yanayonizunguka ni changamoto. Unaweza ukajikinga lakini wenzako wanaokuzunguka wasijikinge na hivyo kukuweka katika hatari ya kupata maambukizi," alisema Hamidu Omari, mfanyabiashara wa Mwenge.

●**Imeandikwa na Mary Geofrey, Sechellah Nakamba na Haika Christopher (SJMC)**

# Samia aonya hujuma ndege za serikali

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameongoza mapokezi ya ndege ya tisa iliyonunuliwa na serikali, akionya hujuma dhidi ya ndege hizo.

Katika hotuba yake wakati wa mapokezi hayo jijini Dar es Salaam jana, Rais Samia alisema ndege hizo zimepatikana kwa jasho na damu, hivyo watumishi wa Shirika la Ndege (ATCL) wanapaswa kuwa makini katika utunzaji na uhudumiaji wake.

Ndege mpya iliyopokewa jana ni aina ya Bombadier DASH 8-Q400, Rais Samia akiagiza: "Kudhibiti vitendo vya hujuma kwa ndege zetu, zikituzwa zitakaa muda mrefu na zitaleta tija ambayo tumeikusudia."

Alisema kwa miaka mitano ijayo wanategemea kuliimarisha shirika hilo pamoja na sekta ya usafiri wa anga.

Kuhusu vikwazo vinavyolikabili shirika hilo, Mkuu wa Nchi alisema serikali imepokea na juzi alipokea mpango kazi wa shirika hilo unaopitiwa na ofisi yake kabla ya kufanya mjadala wa pamoja na ATCL na wizara husika kuona namna watakavyokwenda.

Pia alisema wanalifanyia kazi suala la hisa za asilimia 20 kwenye kampuni inayotoa huduma ya chakula kwenye ndege hizo ili ATCL iwe sehemu ya utoaji wa huduma hizo kwa kiwango kikubwa.

Rais Samia pia alifurahishwa na marubani wanawake wanne waliorusha ndege na watatu wengine watakaojiunga nao hivi karibuni.

Alisema usafiri wa anga ni kichocheo muhimu duniani kwa sababu ni salama na wa haraka.

Rais Samia alisema kwa kutambua hilo, ndiyo sababu Tanzania imeamua kununua ndege ya kusafirisha mizigo kwa kuwa ni miongoni mwa wazalishaji wa matunda, mboga na maua.

"Suala la kuwa na ndege ni muhimu, tunaangalia ukuaji wa uchumi tunaanza na ndege moja, tukikua vizuri mbele tutakuwa na nyingine," alisema.

Rais pia alisema ili nchi ivutie watalii wengi na kunufaika nao, ni lazima iimarishe usafiri wa anga na udhibitisho wanaona nchi zingine zilizojiimarisha katika eneo hilo zikiwamo Morocco, Afrika Kusini, Misri na Kenya.

Alisema mbali na mpango wa ununuzi wa ndege 11, wamejenga rada nne Dar es Salama, Kilimanjaro, Mwanza ili kuimarisha usalama wa anga la Tanzania na kupunguza gharama za uendeshaji.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Ladislaus Matindi, alibainisha baadhi ya vikwazo vinavyowakabili yakiwamo madeni waliyorithi na mlipuko wa virusi vya corona.

"Tunashukuru serikali kwa kuchukua hatua kulipa baadhi ya madeni hayo yakiwamo madeni makubwa," alisifu.

# AZAKI zapewa darasa

**Na Mwandishi Wetu**




Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Vickness Mayao (kulia), Rais wa Shirika la Foundation for Civil Society (FCS), Dk. Stigmata Tenga (wa pili kulia), Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Liliani Badi (wa tatu kulia), Mbunge wa Viti Maalum kupitia mashirika hayo, Neema Lugangira, na Mkurugenzi Mtendaji wa FCS, Francis Kiwanga, wakishuhudia uzinduzi wa Wiki ya Asasi za Kiraia (AZAKI) 2021, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOHN BADI**

MWENYEKITI wa Baraza la Uratibu wa Asasi za Kiraia Taifa (NaCoNGO), amezitaka Asasi za Kiraia (AZAKI) kufanya kazi kwa tija na kufuata sheria, wajibu na weledi ili kuleta maendeleo kwenye jamii.

Lilian Badi aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa wiki ya AZAKI, ulioshirikisha asasi mbalimbali nchini.

Alisema asasi hizo ni muhimu kukutana ili kujifunza na kubadilishana uzoefu na kwamba NaCoNGO itaendelea kushirikiana nazo hususan katika kufanya maboresho na mageuzi kwa mujibu wa sheria.

"Ni muhimu kutambua kwamba Foundation for Civil Society (FCS) imekuwa kinara katika kuzijengea uwezo AZAKI kupitia ruzuku na hata mafunzo mbalimbali.

"Tunapozindua wiki ya AZAKI ni ushahidi wa ufanisi na dhamira ya asasi kufikia mafanikio," alisema Lilian.

Alisema FCS pamoja na wadau wengine wanapaswa kuendelea kuunga mkono NaCoNGO na kutekeleza majukumu yao kisheria na kwamba hatua hiyo itasaidia kupungua kwa migogoro ya mara kwa mara isiyo na tija kwenye asasi ambayo hudhoofisha utendaji.

Mkurugenzi Mkuu wa FCS, Francis Kiwanga, alisema katika kuandaa wiki ya AZAKI itakayoanza Oktoba 25 hadi 29, mwaka huu, wanatarajia kumwalika Rais Samia Suluhu Hassan kuwa mgeni rasmi.

Alisema lengo ni kutathmini kazi zao na kuongeza maeneo ya kimkakati.

"Ili kuleta tija katika maeneo nchini, ni kazi ya serikali lakini serikali haiwezi kufanya peke yake, inatakiwa kila mmoja kuchangia.

"AZAKI tunatakiwa kutoa mchango wetu na nguvu kuelekeza nguvu zetu zaidi hususan kwenye mpango wa taifa wa miaka mitano," alisema.

Aliongeza kuwa wiki hiyo pia itahusisha maonyesho ili jamii izifahamu AZAKI zilizopo nchini na majukumu yao kijamii kwa kila asasi ambayo inatambuliwa na serikali.

Mbunge wa Viti Maalum, Neema Lugangira, alisema AZAKI zikitumia fedha za ruzuku ipasavyo kwenye sekta mbalimbali, itasaidia miradi kuwa endelevu.

"Mara nyingi asasi za kiraia huwa tunahesabiwa kama sekta binafsi, asasi zinasimama katika kuchangia maendekeo na sio katika kupata faida, ninasema hilo kwa sababu nina taasisi.

"Kuna vijana wanafanya kazi kwangu ambao wanaojitolea, ninawalipa posho, TRA inawahesabia kama wafanyakazi na kututoza kodi, tunahitaji sheria sahihi," Neema alishauri.

# Rais Samia ateua mrithi wa Mfugale

**Na Mwandishi Maalum**



RAIS Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi wa viongozi wawili, akiwamo Rogatus Mativila (pichani), aliyeteuliwa kuwa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS).

Mativila anachukua nafasi iliyokuwa wazi kutokana na kufariki dunia kwa Patrick Mfugale Juni 29 mwaka huu.

Taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Jaffar Haniu, Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, ilibainisha kuwa kabla ya uteuzi huo, Mativila alikuwa Mkurugenzi wa Barabara, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi).

Taarifa hiyo ya Ikulu pia ilibainisha kuwa Rais Samia amemteua Profesa Yunus Mgaya kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO).

Profesa Mgaya pia ni Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu.

Taarifa ya Ikulu ilibainisha kwamba uteuzi wa viongozi hao wawili ulianza rasmi Julai 28 mwaka huu.

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

## TANZANIA FOREST CONSERVATION GROUP

### STATEMENT OF RECEIPTS AND EXPENDITURE FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2021

This publication of the Statement of Receipts and Expenditure is made in accordance with regulation 13(a) of the Non-Government Organization Act (Amendments), Regulation 2018 which requires Non-Government Organizations receiving funds exceeding TZS 20 Million to publish bi annually the funds received and its expenditure.

| DETAILS | ACTUAL - TZS |
|---|---|
| **RECEIPTS** | |
| Opening fund balance | 1,705,440,505.00 |
| Disbursement from Donors | 452,211,058.00 |
| **TOTAL RECEIPTS FROM DONORS** | **2,157,651,563.00** |
| | |
| **PROGRAMMES EXPENDITURE** | |
| Participatory Forest Management | 100,417,774.00 |
| Environmental Education | 104,515,236.00 |
| Community Development (Poverty reduction in rural communities) | 424,024,941.00 |
| Communication and Advocacy | 104,160,433.00 |
| **OTHER PROGRAMME EXPENDITURE** | |
| Institution Development and Resources Mobilization | 186,385,957.00 |
| Personnel | 668,862,929.00 |
| **TOTAL PROGRAMMES EXENDITURES** | **1,588,367,270.00** |
| **FUND BALANCE**** | **569,284,293.00** |

****Fund balance represents an obligation to conduct donor funded activities per contractual commitments made between donor/development partners and the organisation/recipient, where funds have not been transferred and such activities have not yet occurred.**

**Executive Director**
**Tanzania Forest Conservation Group**
**Plot 323, Msasani Village**
**Mwaikibaki Rd**
**P.O. Box. 23410**
**Dar es Salaam**
**Tanzania**

216386702

## RIPOTI MAALUM - IV

# Mauaji wivu wa mapenzi yanavyoacha simanzi

**Na Maulid Mmbaga**

**SEHEMU ya tatu ya ripoti hii iliangazia matukio mbalimbali ya mauaji kwa mwaka jana na kuonyesha kwa sehemu kubwa yalichagizwa na wivu wa mapenzi. Endelea na sehemu ya mwisho...**

JANUARI Mosi mwaka huu, mkazi wa kijiji cha Pemba wilayani Tarime mkoani Mara Burure Mniko alishikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kumuua baba yake mdogo aitwaye Chiranye Mniko, chanzo ni ulevi.

Januari 3, mkazi wa Kitongoji cha Kwasalaka, wilayani Kilindi, mkoani Tanga, Seif Hatibu, alidaiwa kumuua kaka yake Mahimbo Hatibu, chanzo ni ugomvi unaotajwa kusababishwa na deni la Sh. 13,000.

Januari 4, Polisi mkoani Kagera walimshikilia Amos Ludovick (39) mkazi wa kijiji cha Ibale, wilayani Kyerwa kwa madai ya kusababisha kifo cha mtoto wake Dastan Amos (13), kutokana na fimbo.

Siku hiyo pia, mwanafunzi wa Shule ya Royal Vision ya jijini Arusha, Junior Calvin (11), alidaiwa kukatisha uhai wake kwa kujinyonga na kipande cha kamba ya sweta.

Januari 5, Ben Maganga (26), alitiwa hatiani kwa kumbaka na kumpa mimba mwanafunzi wa kidato cha kwanza mwenye umri wa miaka (15).

Januari 10, mwalimu wa Shule ya Msingi Namibu B, Halmashauri ya Bunda mkoani Mara ambaye jina lake halikubainishwa alikamatwa kwa kosa la ubakaji.

Januari 14, polisi mkoani Ruvuma lilimshikilia mfanyakazi wa kampuni ya ulinzi ya Komesha, Shabani Mpacha, kwa tuhuma za kumuua mke wake Zainabu Yassin (46) kwa madai ya wivu wa kimapenzi.

Januari 18, askari polisi Yusuph Said (52), na msichana wa kazi Chausiku Rashidi (20) walikutwa wamekufa kwa kujinyonga, tukio lililotokea Kibaha mkoani Pwani na Kitunda jijini Dar es Salaam.

Januari 19, mkazi wa mtaa wa Julia Newala mkoani Mtwara, Hashimu Suleimani, alifariki dunia baada ya kujimwagia mafuta ya Petroli mwilini na kujichoma moto hadharani kwa wivu wa kimapenzi.

Januari 22, mkazi wa Wilaya ya Ludewa mkoani Njombe Claus Lugome, alidaiwa kumuua ndugu yake Rainary Lugome, kwa madai ya kuku wake waliingia katika shamba la kaka yake.

Januari 25, mfanyakazi wa ndani mwenye umri wa miaka (19) alituhumiwa kumuua mtoto wa bosi wake Heleni Chistopher (10) mkazi wa Kawe Mzimuni mkoani Dar es Salaam.

Tarehe hiyo pia katika Jiji la Arusha, mkazi wa kijiji cha Olosiva Kata ya Olorieni jijini humo Olaisi Wavii (46) alishikiliwa na polisi kwa madai ya kumnajisi mtoto wake wa miaka mitatu.

Januari 26, Samuel James, mkazi wa mtaa wa Mageuzi, Kata ya Ndembezi Shinyanga kumuua mke wake, Paulina Daudi kwa kumpiga na mtwangio kutokana na ugomvi wa kifamilia.



Januari 27, kijana Pawa Kandago (22) mkazi wa kijiji cha Mapogoro mkoani Mbeya, alidaiwa kujinyonga kutokana na mifugo yake ng'ombe zaidi ya 50 kukamatwa na vikosi vya ulinzi na usalama bonde la Ihefu.

Februari 4, Ahamadi Makotta (43) mkazi wa kitongoji cha Majengo, alituhumiwa kumuua kaka yake Abdull Makotta (55) kutokana na ugomvi uliosababishwa na kugombea nyumba ya urithi iliyoachwa na marehemu baba yao.

Februari 7, polisi mkoani Shinyanga liliwashikilia wanandoa wawili Christina Mwangi na mume wake Yohana Michael kwa tuhuma za kumchoma moto mtoto wao na kumsababishia majeraha, kwa madai ya kuiba karanga.

Februari 9, Jackson Bahati (27) mkazi wa kijiji cha Buhangizi, Kata ya Kagu, mkoani Geita, alidaiwa kuwajeruhi watoto wake wawili kwa kuwachoma kisu maeneo ya tumboni baada ya kubaini kuwa aliyekuwa mke wake ameolewa na mwanaume mwingine.

Februari 13, mwanafunzi wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Ndugu wilayani Mbozi mkoani Songwe, Rehema Kapufi (15) alijinyonga.

Machi mosi, Ally Mkonga (58) mkazi wa Kata ya Raheleo Manispaa ya Lindi ambaye pia ni mwalimu wa madrasa alihukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 20 kwa kosa la udhalilishaji kingono.

Machi 5, Deus Kakusu (52), Mkazi wa Kijiji cha Kanazi Kata ya Ntatumbila wilayani Nkasa, mkoani Rukwa, alidaiwa kujinyonga hadi kufa kwa kutumia chandarua, kwa sababu zilizotajwa kuwa ni ugumu wa maisha.

Tarehe hiyo hiyo, Mtawa wa kituo cha kuhudumia wagonjwa wa Ukoma cha Nazareth kilichopo Ifakara mkoani Morogoro, Agatha Mbalalila (50) aliuawa kwa kuchomwa kisu na mgonjwa aliyekuwa akipatiwa matibabu katika kituo hicho.

Machi 10, Polisi mkoani Mbeya lilimshikilia Mussa Benard (27) na wenzake wawili kwa tuhuma za kumuua mume na mke.

Machi 14, Sikonge mkoani Tabora watu wasiojulikana walidaiwa kuwaua mwanafunzi na dereva bodaboda katika matukio tofauti na miili yao kuitelekeza vichakani, na sababu za tukio hilo hazikubainishwa.

Machi 22, Mkazi wa Handeni mkoani Tanga, Christopher William, alidaiwa kumuua kikatili rafiki yake kwa kumcharanga na mapanga kutokana na deni la Sh. 3,000.

Machi 25, Mahakama Kuu Tanzania, Kanda ya Mwanza iliwahukumu watu 14 kunyongwa hadi kufa baada ya kukutwa na hatia ya kusababisha mauaji ya watu katika sehemu mbalimbali kwa kukusudia.

Machi 27, mkoani Dar es Salaam, watu wasiojulikana walimuua aliyekuwa mwandishi wa habari wa ITV/Radio One na mtangazaji wa kipindi cha jarida la wanawake Blandina Sembu (47) na sababu za kutokea kwa tukio hilo hazikubainishwa.

Aprili 2, mkoani Tarime, watu wasiojulikana walisababisha vifo vya watu wawili katika matukio tofauti, akiwamo Mwenyekiti wa Mtaa, Juma Kamugisha ambaye alichomwa na kitu chenye ncha kali tumboni.

Tukio lingine ni la mlinzi wa duka Nyamhanga Mwita, aliyeuawa kwa kukatwa na mapanga wakati akiwa katika lindo lake usiku.

Aprili 6, mwanafunzi wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Kahororo Bukoba, Irene Revocatus (10) aliuawa kwa kupigwa na kitu kizito kichwani, kubakwa kisha kutupwa kichakani na watu wasiofahamika.

Aprili 9, mkazi wa kijiji cha Janda Buhigwe mkoani Kigoma Shinje Mugalama, aliuawa kikatili na watu wasiojulikana kwa kukatwa shingo na kutenganishwa na kiwiliwili.

Aprili 13, mama mwenye umri wa miaka 41 mkazi wa Mvumero, mkoani Morogoro, alibakwa na vijana tisa aliodai kuwa ni jamii ya Kimasai.

Aprili 16, Joachim Rwegasira (45) mkazi wa kijiji cha Buhanga, Muleba mkoani Kagera, alishikiliwa na polisi kwa tuhuma za kumuua mke wake na mtoto wa mwaka mmoja kwa madai kuwa mke wake alikuwa na mahusiano ya kimapenzi na jirani yake.

Aprili 18, mkazi wa kitongoji cha Butiama wilayani Kyela, Amini Sanga (36) alitiwa mbaroni kwa tuhuma za kumuua mkewe Mariam Mahenge (25) kwa kumcharanga mapanga kwa madai ya wivu wa mapenzi.

Aprili 25, polisi mkoani Pwani lilimshikilia Askari wa jeshi la wananchi wa Tanzania, Praiveti Godfrey kwa tuhuma za kumchoma kisu hadi kufa mke wake Fatuma Salumu, kwa madai ya kufanya tendo la ndoa nje ya ndoa.

**ITAENDELEA**


**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(COMMERCIAL DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**
**COMMERCIAL CASE NO. 4 OF 2021**
**ALIOS FINANCE TANZANIA LIMITED.............................PLAINTIFF**
**VERSUS**
**AHMED ALLY HEMED ................................................DEFENDANT**
**DECREE:**

**WHEREFORE,** the Plaintiff prays for judgment and decree as follows:

a) A declaration that the Defendant breached of the Vehicle Lease Agreement dated 21st September, 2017.
b) Payment of TZS 185,360,298.79/= being outstanding amount arising from the unpaid installment arrears, remaining principal amount and late fees penalties arising from the vehicle leasing agreement.
c) Payment of interest at the commercial rate prevailing at the date if Judgment or such rate as the Honorable court may deem fit and just, accruing and computed from the date of the judgment of this suit.
d) Payment of General damages as may be assessed d by this Honorable Court
e) Payment of the cost of this suit and
f) Any other relief(s) that the Honorable Court may deem fit and just to grant.

This suit is coming up for Consent Judgment on 13th day of July, 2021, before His Lordship, Mr. Justice Dr. D.J. Nangela, Judge in the presence of Mr. David Kasanga hold brief of Ms. Esther Peter, Advocate for the Plaintiff and in the absence defendant.

**THIS COURT DOTHE HEREBY ORDER THAT:**

The judgment in default is here entered in favour of the Plaintiff and order as follows;

a) It is hereby declared that, the Defendant breached the Vehicle Lease Agreement dated 21st September ,2017;
b) The Defendant shall, without failure, pay the Plaintiff TZS 185,360,298.78/= being outstanding amount arising from unpaid installment arrears and the remaining principal amount arising from the vehicle lease agreement.
c) Defendant shall pay interest at the Commercial rate of 14% from the date of Judgment to the date of final payment thereof.
d) The defendant shall pay the Plaintiff TZS 5,000,000 as general damages.
e) The Defendant shall pay interest at the Court rate of 7% of the decretal amount from the date of this judgment to the date when the decree is fully satisfied.
f) The defendant shall pay costs of suit.

Given under my hand and the seal of the Court this day of 13th day of July, 2021.

..........................................................................
**Dr. D Nangela,**
**JUDGE, HIGH COURT OF TANZANIA**
**(COMMERCIAL DIVISION)**
**13th day of July, 2021**
**Extracted on 13th say of July, 2021**

216387202

# Viongozi wakiukaji maadili kushughulikiwa

**Na Romana Mallya**

JUMUIYA ya Maridhiano Tanzania imetangaza kuwashughulikia wanachama na viongozi wasio na maadili na wanaokiuka katiba ambayo wameifanyia mabadiliko.

Taarifa ya jumuiya hiyo ambayo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Naibu Katibu Mkuu, Dk. Abdulrazak Juma, ilisema hilo ni miongoni mwa maazimio manne yaliyofikiwa juzi katika mkutano mkuu wa maridhiano ambao pamoja na mambo mengine, umefanya mabadiliko ya katiba.

Dk. Juma alitaja maazimio mengine kuwa ni jumuiya kuendelea kuiunga mkono serikali kuhusu juhudi zake za kuwapatia Watanzania chanjo iliyo salama dhidi ya corona.

"Jumuiya itaendelea kushirikiana na serikali katika kazi ya kudumisha amani na utulivu, kushirikiana na taasisi zote zenye nia na dhamira njema kwa Watanzania," alisema.

Sambamba na hilo, alisema mkutano mkuu umemchagua Sheikh Alhad Mussa Salum kuwa mwenyekiti wa taifa wa jumuiya.

"Dk. Elias Silayo amechaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu Askofu Israel Maasa na Naibu Katibu Mkuu Dk. Abdulrazak Juma, mshauri wa mambo ya kijamii, Dk. Nurdin Mangochi, Mratibu Jovent Bitibiye, Mshauri wa kisheria Bibie Msumi, mkuu wa mila na desturi, Dk. Ester Kroll na mlezi ni Mizengo Pinda," alisema.

Aliwataja wajumbe 10 waliochaguliwa ni Primo Andriano, Sheikh Swedi Twalib, Sheikh Yahya Mkumba, Amina Mkumba, Festo Kilawe, Dk. Evance Chande (Askofu), Sheikh Said Abri, Askofu Stanley Hotay, Chief Fundikira na Askofu Joel Lugan.

Alisema mkutano mkuu umemwachisha uongozi na kumfukuza uanachama Mchungaji Oswald Mlay.

Alisema mkutano mkuu umethibitisha majina ya wadhamini 10 ambao wamependekezwa na kamati kuu ambao ni Gaundance Lyimo, Sheikh khamis Mataka, Salim Muhsin, Lazaro Mambosasa, Suleiman Kova, Philip Mpango, Francis Mutungi, Azim Dewji, Katibu Mkuu na Dk. Tulia Akson.

Pia alisema kamati kuu imeteua viongozi wa mikoa 16 kwenye nafasi ya mwenyekiti, makamu mwenyekiti, katibu na Naibu Katibu.

Aliitaja mikoa hiyo kuwa ni Dodoma, Arusha, Mtwara, Morogoro, Kilimanjaro, Mwanza, Tanga, Pwani, Kigoma, Simiyu, Dar es Salaam, Tabora, Mbeya, Iringa, Kagera na Singida.

Mwenyekiti wa jumuiya hiyo, Sheikh Musa alisema awali jumuiya ilikuwa ikiyumba, haiendi vizuri na kuishia kulalamikiwa.

Alisema baada ya mabadiliko hayo yaliyofanyika ikiwa ni pamoja na kubadilisha katiba, itakuwa imara na kuimarika.

"Tutaendelea kushirikiana na serikali katika mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na migogoro mbalimbali iliyopo ikiwamo ya wakulima na wafugaji," alisema.

Askofu Maasa alisema watashirikiana na viongozi wa mikoa ili kuona mikoa ambayo bado haijapata viongozi wa jumuiya hiyo iweze kuwa nao.

Naye Dk. Silayo alisema maazimio waliyofikia yanalenga kujenga upya jumuiya ili kudumisha na kuimarisha amani.

# Jafo aiangukia NMB elimu, afya

**Na Julieth Mkireri,** KISARAWE

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, ameiomba Benki ya NMB kuendelea kuisaidia serikali masuala ya kijamii ili kuondoa vikwazo vya maendeleo vilivyopo.

Jafo ameyasema hayo jana mjini hapa alipokuwa akipokea msaada wa viti 50 na meza pamoja na mabati 160 kwa ajili ya Shule ya Msingi Chanzige na Sekondari ya Mzenga vyenye thamani ya Sh. milioni 10 vilivyotolewa na benki ya NMB.

Jafo ambaye pia ni Mbunge wa Kisarawe, alisema benki hiyo imekuwa ikisaidia mambo mengi ya kijamii katika wilaya ya Kisarawe na kwa ushirikiano huo imekuwa ikiisaidia serikali katika elimu na afya.

"NMB msituchoke mmetusaidia mambo mengi ikiwamo hili la leo ambalo niliwaomba hivi karibuni tukiwa hapa katika Shule ya Msingi Chanzige. Huko vijijini tunahamasisha ujenzi wa vituo vya afya, mnapoweza mwendelee kutusaidia vifaa," alisema Jafo.


Aidha, Jafo aliomba benki hiyo kufungua tawi katika maeneo ya Manerumango na Mzenga ili kuwasogezea wananchi huduma hiyo karibu na maeneo wanayoishi.

"Manerumango inakua siku hadi siku. Wafanyabiashara sasa ni wengi na wapo wafanyakazi walimu na watendaji wanahitaji huduma za kibenki karibu na eneo hilo. Liangalieni hili mfanye utaratibu wa kuwafungulia tawi," alisema.

Mkuu wa Kitengo cha Biashara za Serikali cha NMB, Vicky Bishubo, alisema kwa mwaka huu benki hiyo imetenga zaidi ya Sh. bilioni mbili kwa ajili ya maendeleo ya jamii ikiwamo kisaidia elimu na afya.

Alisema hadi sasa wametoa misaada yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni moja kwa mwaka huu na msaada walioukabidhi umegharimu Sh. milioni 10.

Bishubo alisema mbali na misaada hiyo kwa jamii pia wamekuwa wakiwezesha vijana kupata elimu ya fedha na kuweka akiba katika umri mdogo kupitia programu ya 'Jifunze, Jipange, Wajibika'.



Mbunge wa Viti Maalum na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Munde Tambwe, akipata chanjo ya kujikinga na virusi vya corona, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Agundua mfumo wa kusaidia wagonjwa shinikizo la damu

**Na Romana Mallya**

BAADA ya kuona mateso anayopitia baba yake, mbunifu Sadiki Godfrey amebuni mfumo wa kusaidia wenye shinikizo la damu ambao utasaidia ndugu kupata taarifa pindi wanapoziidiwa.

Godfrey ambaye ni mwanafunzi wa Stashahada katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Dar es Salaam, alisema ili mfumo huo utumike mhusika atounganishwa na ndugu ambao watakuwa wanapata ujumbe mfupi kupitia simu zao za mkononi.

Kijana huyo aliyasema hayo jana katika maonyesho ya 16 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia yaliyoandaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).

Alisema alilazimika kubuni mfumo huo baada ya baba yake mzazi kuwa anasumbuliwa na tatizo hilo kila mara na hali imekuwa ikibadilika na wakati mwingine akiwa peke yake.

"Niliamua nibuni mfumo huu ili kusaidia watu wanaosumbuliwa na matatizo haya ili hata kama watakuwa peke yao na hali ikawabadilikia, wapate msaada wa haraka. Mfumo utatuma ujumbe mfupi kwa ndugu kuwa amezidiwa," alisema.

Alisema tayari ameshafanya majaribio kwa mwanafunzi anayesoma chuoni hapo ambaye ana tatizo la shinikizo la damu na ukaleta matokeo chanya.

"Mfumo huu ambao mhusika atauvaa kama saa, utakuwa unampima shinikizo la damu. Kama mhusika atakuwa na tatizo wakati akiendelea na shughuli zake, atapata ujumbe mfupi kwenye simu yake pamoja na ndugu ambaye atounganishwa kwenye mfumo ili apate huduma ya haraka," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF, Bodi ya Ligi andaeni ratiba rafiki msimu mpya

**SHIRIKISHO** la Soka Nchini (TFF), tayari limeshafungua dirisha la usajili wa wachezaji ambao watashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Pili na Ligi Kuu ya Wanawake kwa ajili ya msimu mpya wa 2021/2022.

Kwa upande wa Ligi Kuu Tanzania Bara, msimu ujao utakuwa na timu 16 ambazo ni mabingwa Simba, Yanga, Azam, Biashara United, Namungo, KMC, Polisi Tanzania, Kagera Sugar, Dodoma Jiji, Ruvu Shooting, Mbeya City, Tanzania Prisons, Mtibwa Sugar, Coastal Union, Mbeya Kwanza na Geita Gold FC.

Usajili huo utafungwa rasmi ifikapo Agosti 31, mwaka huu na TFF imesisitiza klabu zote kuzingatia kalenda hiyo kwa sababu hakutakuwa na muda wa nyongeza katika kukamilisha mchakato huo muhimu.

Ili kufanya vyema katika msimu ujao, klabu zote zinakumbushwa kufanya usajili mzuri ili kuwa na vikosi imara ambavyo vitaonyesha ushindani na si kuwa wasindikizaji kwenye ligi hizo na mashindano mengine ya ndani na nje ya nchi watakayoshiriki.

Timu pia zinakumbushwa kuboresha mabenchi ya ufundi kwa kuajiri makocha wenye sifa na uzoefu wa kushiriki ligi hizo pamoja na mashindano ya kimataifa kwa klabu nne ambazo msimu ujao zitapeperusha bendera ya Tanzania kwenye michuano inayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Klabu zikumbuke kufanya usajili kwa kufuata mapendekezo ya kiufundi waliopewa na makocha walioziongoza timu hizo na kuacha kusajili wachezaji kwa kusikiliza 'kelele' za mashabiki wao ambao kiufundi hawana nafasi.

Nipashe inazikumbusha klabu kusajili wachezaji ambao watakwenda kuimarisha vikosi vyao na si kwenda kusotea benchi, lakini hili pia likibakia kwenye uamuzi wa wachezaji husika ambao hukubali kuweka saini katika timu ambazo wanafahamu kupata namba ya kucheza ni kitendawili.

Umefika wakati wa kuwakumbusha wachezaji wetu kufanya uamuzi wa kujiunga na timu itakayomsaidia kuendeleza kipaji chake na si kuzingatia kipengele kimoja tu cha maslahi, kama ambavyo tumeshuhudia kwa baadhi ya nyota wakipotea, hali ya kuwa walitarajiwa kulitangaza taifa vyema ndani na nje ya Tanzania.

Baada ya klabu kukamilisha mchakato wa usajili kwa usahihi na kukamilisha programu za mazoezi vyema, sasa kilichobaki ni kwa wasimamizi TFF kupanga ratiba rafiki ambayo haitaumiza wachezaji wetu kama ambavyo tumeshuhudia katika misimu miwili iliyopita.

TFF inatakiwa kuhakikisha inatoa ratiba rafiki itakayowapa wachezaji nafasi ya kupumzika na kuonyesha viwango vyao halisi na si kwenda vituoni kukamilisha ratiba hizo.

Tayari inafahamika msimu ujao ambao utaanza mapema Septemba, mwaka huu, Tanzania itawakilishwa na timu nne katika mashindano ya CAF, TFF isione aibu kuomba msaada kwa nchi zilizoendelea katika kusaidia au kushauri upangaji wa ratiba ili suala la klabu moja kuwa na idadi kubwa ya mechi za viporo lisijirudie.

Mechi za viporo zinapokuwa nyingi, hupunguza ushindani lakini huruhusu malalamiko yasiyo na msingi kwa sababu baadhi ya mechi huchezwa kwa kukamilisha ratiba na jambo hilo hupunguza ushindani, lakini vile vile linaweza 'kuamsha' upangaji wa matokeo.

Pia tunakumbusha ratiba hiyo isisahau kuzingatia jiografia ya Tanzania na hali halisi ya kiuchumi ya klabu zetu kwa kujaribu kuzipangia kucheza mechi zote inapokwenda kwenye ukanda mmoja. Hii itasaidia timu kucheza kwa amani na vile vile kupata muda wa kufanya mazoezi kila baada ya kumaliza mchezo mmoja.

Tunaendelea kuwakumbusha Ligi Kuu Tanzania Bara ndio tegemeo kubwa la Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Kim Poulsen kupata wachezaji ambapo hupeperusha bendera ya nchi katika mashindano mbalimbali, hivyo kuifanya ligi hiyo kuchezwa kwa mtindo wa bora liende, itakuwa tu si kuziumiza klabu, lakini pia itaidhoofisha Stars.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Fedheha za mwezio usizifurahie

Na Barnabas Maro

**SIO** tabia njema kufurahia aibu au fedheha zilizomfika mwenzio. Methali hii huweza kutumiwa kutunza umuhimu wa kutowacheka wenzetu wanapopatwa na matatizo kwa kuwa tunaweza kupatwa na matatizo hayo. Leo ni kwako kesho ni kwetu. Methali hii inawafaa wasemaji wa timu za Simba na Yanga.

Leo natumia methali zaidi ili wanaojiona wanahusika wajirekebishe kwani kila neno lina kipindi chake. Maana yake kila neno lina wakati wake au kipindi ambapo linasibu au linafaa.

Methali hii hutumiwa kumwerevusha mtu anayesema maneno fulani pasipofaa au pasipohitajika. Pia huweza kutumiwa kutukumbusha kuwa kila jambo lina wakati wake; hamna linalofanyika likafanana kabla ya wakati wake kufika.

Wahenga walituachia methali isemayo. "Leo kwako kesho kwa mwenzio" wakiwa na maana kuwa jambo linalokupata leo, liwe la shida au la raha huweza kumpata mwenzio kesho. Methali hii hutumika kutunasihi tusiwacheke wenzetu wanapokumbwa na matatizo kwa kuwa yanaweza kutukumba na sisi pia.

Huweza kutumika kumtanabaisha mtu anayejitapa kwa kuwa na hali nzuri kuwa kesho anaweza asiwe na hali hiyo na badala yake awe nayo mwenzake aliyemdharau.

Aidha "Leo ni yako kesho sio." Mtu huwa na hakika na wakati alionao bali sio wakati ujao. Pia "leo ni siku yako lakini kesho ni ya mwenzako." Methali hii yalingana na ile ya "Leo kwako kesho kwa mwenzio."

Tunaambiwa pia "Liandikwalo pia halifutiki." Maana yake jambo ambalo limeandikwa na Mungu lifanyike lazima lifanyike, haiwezekani kufutika. Methali hii hutumiwa kumliwaza mtu aliyefikwa na maafa au msiba fulani kwamba hayo ni mapenzi ya Mungu.

Wakati Yanga ilipoifunga Simba goli 1- 0 kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, kuna binadamu aliyejitangaza kuwa ushindi wa Yanga ulitokana naye kwani alikuwa na watu watatu akiwa na maana ya watu ambao ndio waliosababisha ushindi wa Yanga!

Alisema kuwa ndiye aliyekuwa na waganga watatu walioiwezesha Yanga kuifunga Simba bao 1-0 jijini Dar es Salaam. Akajitapa kuwa timu hizo zitakapokutana kule Kigoma, Yanga ingeifunga tena Simba kwa mabao mengi. Pamoja na kujiamini kote huko kibao kikageuka kwa Yanga kufungwa bao 1-0 kule Kigoma hivyo Simba kutwaa Kombe la FA/Shirikisho (ASFC) kwa mara ya pili mfululizo.

Nikakumbuka ile methali isemayo "Simba mwenda pole (kimya) ndiye mla nyama." Maana yake Simba aendaye taratibu bila kujitambulisha ndiye anayeweza kuwakamata (shika wanyama bila shida.) Methali hii yatunasihi tuwe na utaratibu katika utendaji wetu wa mambo tusiwe na tabia ya kuyapapia mambo.

Katika pitapita zangu niliona kundi la watu wakibishana baada ya mechi ya Simba na Yanga mjini Kigoma. Mmoja wa watu hao alisema kwa kujiamini kuwa Simba haikutaka kuwachosha wachezaji kwani mchezo ule wa Dar es Salaam haukuwa na maana yoyote kwao hivyo ikawaachia Yanga ili ishinde!

Mashabiki wa Simba wakashangilia sana, wakisema wachezaji walikuwa wanasubiri mechi ya Kigoma kwani ndio ilikuwa ya maana kwao.

Mwingine akakubaliana na msemaji aliyetangulia aliposema timu yake (Simba) haikutaka kuwachosha wachezaji kwa mchezo usiokuwa na faida ila walitaka kuisaidia Yanga imalize Ligi Kuu kwa ushindi ili iisindikize Simba kutwaa Kombe la Shirikisho (ASFC) Kigoma kwa mara ya pili mfululizo.

Napenda kuwazindua wanachama na mashabiki wa Simba na Yanga kuwa wao ni ndugu wanaoishi Tanzania katika jiji lililoitwa 'Bandari ya Salama' zamani ambalo sasa ni Dar es Salaam maeneo ya Kariakoo. Kwa nini wazishangilie timu ngeni zitokazo nje ya Tanzania zinapokuja nchini kushindana na timu hizo?

Ujinga ni hali ya kukosa kujua kitu fulani. Kwa maneno mengine ni ubozi, ubwege. Kwa nini tunakuwa wajinga kiasi hiki? Twapaswa kutambua kuwa ubaya hatima (mwisho wa jambo baada ya muda au kipindi fulani) yake mbaya. Twahimizwa tuwe na nia nzuri au tusiwafanyie wenzetu mambo mabaya.

Yale yasemwayo mara kwa mara kuwa Simba na Yanga ni "Watani wa jadi" sikubaliani nao kwa jinsi mashabiki wao wanavyofanyiana unaa, yaani tabia ya kupenda kuwatilia fitina watu wengine timu za Simba na Yanga zinapopambana na timu za ughaibuni zinapokuja kwetu!

Hata hivyo, nadhani kile kitwacho 'watani wa jadi' baina ya Simba na Yanga sasa inaanza kueleweka kwenye baadhi ya mikoa yetu. Mfano, Yanga ilipoifunga Simba bao 1-0 jijini Dar es Salaam wapenzi wa Yanga wa Kibirizi mkoani Kigoma waliwanyoa nywele wenzao wa Simba na Yanga ilipofungwa na Simba kule Kigoma ilikuwa zamu ya wapenzi wa Simba kuwanyoa wenzao wa Yanga, kuwapaka poda na kuchoma jezi zao za Yanga na kuwavisha jezi za Simba bila matata. Huo ndio utani wa jadi.

Jijini Dar es Salaam, hususani Kinondoni, Simba ilipotwaa Kombe la ASFC kule Kigoma, mashabiki wake waliandaa chakula na kuwakaribisha wenzao wa Yanga kula pamoja nao huku wakirushiana maneno ya hapa na pale, wakichekana na kufanyiana masihara yaani dhihaka. Huo ndio utani wa jadi.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

HABARI KITAIFA

# Dk. Mwinyi aagiza kuondoa kodi kero

**Na Mwandishi Wetu,**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi, amesema kipaumbele cha serikali yake hususani katika sekta ya mafuta na gesi, utalii, uvuvi, biashara na uwekezaji ni katika uchumi wa bluu.

Amesema anaamini uchumi huo utamsaidia Mzanzibari katika kuimarisha kipato huku akisisitiza kuondoa kodi kero kwa wananchi.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi wakati alipokutana na kufanya mazungumzo na uongozi wa juu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ulioongozwa na Waziri Liberata Mulamula kwa lengo la kujitambulisha na kupokea maelekezo ya kutekeleza vipaumbele vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Aliielekeza Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kutilia mkazo katika uwekezaji wa maeneo ya uchumi wa bluu katika mazungumzo na mashirika ya fedha duniani ikiwamo IMF na Benki ya Dunia ikiwa ni pamoja na wawekezaji na wafadhili mbalimbali kwa kuwa serikali yake ina imani kuwa bahari ikitumiwa vizuri, itainufaisha Zanzibar kiuchumi kuliko maeneo mengine.

Dk. Mwinyi pia aliitaka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuwasaidia wafanyabiashara kutoka Zanzibar kuwaunganisha na wafanyabiashara na wawekezaji kutoka nje ili Zanzibar nayo isafirishe bidhaa zake za ndani kwenda nje badala ya kupokea bidhaa kutoka mataifa mengine kama ilivyo sasa.

Alizitaja bidhaa kutoka Zanzibar zinazoweza kusafirishwa nje ya Zanzibar kuwa ni pamoja na karafuu, samaki na nyama ambazo zina soko kubwa nje ya nchi husussani katika nchi za Kiarabu.

Mbali na hilo, Dk. Mwinyi pia aliagiza kupitia upya kwa Sera ya Mambo ya Nje hususani katika suala la Wazanzibar wanaoishi nje maarufu kama Diaspora kupatiwa hadhi maalum itakayowawezesha kushiriki katika uchumi wa nchi ikiwamo kuwekeza, kubadilishana uzoefu wa kitaaluma na masuala mengine ya maendeleo.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mulamula, alisema Wizara imeyapokea maelekezo ya Rais Dk. Mwinyi na tayari kuna mkakati na maelekezo maalum kwa mabalozi wanaoiwakilisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mataifa mbalimbali duniani ili kuhakikisha uhusiano wa Tanzania na nchi hizo unakuwa wa manufaa katika uchumi wa pande zote za Jamuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika ziara yake Zanzibar, Balozi Mulamula na ujumbe wake walikutana na kufanya mazungumzo na Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud, ambaye alibainisha nia ya ofisi yake kupambana kudhibiti biashara na matumizi ya dawa za kulevya pamoja na suala la mazingira ambayo kwa kiasi kikubwa yameathirika kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Katika ziara hiyo Balozi Mulamula aliambatana na Naibu Waziri, Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, Katibu Mkuu, Balozi Joseph Sokoine, Naibu Katibu Mkuu, Balozi Fatma Mohammed Rajab, pamoja na baadhi ya wakurugenzi wa idara na vitengo vya wizara hiyo.



Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Chuo Kikuu cha Mount Kenya, Boniface Murigi (kulia), akifafanua jambo kuhusu huduma zitolewazo kwenye chuo hicho, kwa mwananchi aliyetembelea Maonyesho ya 16 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia yanayoendelea katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. Wa (pili kulia) ni Msimamizi wa Tovuti ya chuo hicho, Rose Macharia. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# JWTZ, Marekani wajifunza vita ugaidi, dawa kulevya

**Na Gwamaka Alipipi**

VIKOSI vya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kwa kushirikiana na vya Jeshi la Marekani Kamandi ya Afrika wameanza mafunzo kwa vitendo yenye lengo la kupambana, kudhibiti matukio ya ugaidi na biashara za dawa za kulevya.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo jijini Dar es Salaam juzi, Mnadhimu Mkuu wa JWTZ, Luteni Jenerali Mohammed Yakubu Mohamed, alisema mafunzo hayo yatatolewa na askari wa Jeshi la Marekani kwa askari wa JWTZ, yatadumu kwa muda wa mwezi mmoja.

Luteni Jenerali Yakubu alisema: "Tangu miaka ya nyuma JWTZ na Jeshi la Marekani yamekuwa na mahusiano mazuri, Jeshi la Marekani limekuwa ni mdau mkubwa kwa JWTZ. Tumekuwa tukishirikiana katika operesheni na mafunzo mbalimbali."

Aliongeza kwamba mbali na kupambana na ugaidi, dawa za kulevya, mafunzo hayo pia yataongeza maarifa na ujuzi kwa askari wa JWTZ watakaopata mafunzo hayo.

Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Marekani, Afrika, Jenerali Stephen Townsend, alisema mafunzo hayo yataongeza ushirikiano baina ya Tanzania na Marekani uliokuwapo tangu enzi.

Alisema mahusiano ya Tanzania na Marekani yalijengwa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere na Rais wa Marekani, Hayati John Kennedy.

Jenerali Townsend alisema: "Mafunzo kwa vitendo yatakuwa ya mwezi mmoja, watajifunza namna ya kupambana na maharamia, vitendo vya uhalifu, pamoja na matukio yote mabaya ambayo yatahatarisha usalama wa nchi."

## 'Vijana changamkieni taaluma kodi, forodha'

**Na Christina Mwakangale**

CHUO cha Kodi (ITA), kimetoa wito kwa vijana kusomea taaluma ya forodha na kodi, kutokana na mahitaji na mkakati wa nchi katika kukuza mapato, uchumi na kupunguza utegemezi.

Ofisa Mkuu Uhusiano wa Umma, Oliver Njunwa, akizumgumza kwenye Maonyesho ya 16 ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, alisema Chuo cha ITA ndicho pekee Afrika Mashariki na Kusini chenye ithibati ya mafunzo ya forodha na kodi.

Njunwa alisema wanafunzi watakaosomea taaluma ya forodha na kodi kujiunga na chuo hicho ambacho kimebobea katika kutoa taaluma hiyo takribani miaka 14 Afrika Mashariki, watatoka na ujuzi mahiri.

"Tunawakaribisha vijana, wazazi, wananchi wote kutembelea banda letu Mnazimmoja, kupata maelezo ya kozi pamoja na kuwasaidia kutuma maombi chuoni," alisema Njunwa.

"Taaluma ya forodha na inahitajika zaidi wakati Tanzania ikiendelea kukuza mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi na kwamba vijana wanaohitimu watasaidia kufanikisha lengo hilo."

Njunwa alisema wanafunzi hao watachagua kozi inayowafaa kutokana na sifa walizonazo na kwamba ambao hawajafikia vigezo vya kujiunga na ITA wanaelekezwa katika vyuo vingine.

"Kwa wale wanaodhani kwamba ukisoma ITA lazima ufanye kazi Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) tunawaeleza kwamba kuna fursa nyingine nyingi za kufanya kazi ambazo mhitimu wa ITA anazipata.

"Anaweza kujiajiri mwenyewe kwa kufungua kampuni yake ya ushauri wa masuala ya kodi na akaajiri wengine, anaweza kuajiriwa katika taasisi za serikali, kwenye kampuni binafsi na hata katika mashirika yasiyokuwa ya serikali (NGOs)," alisema Njunwa.

Alibainisha kuwa chuo kinatoa mafunzo ya umahiri katika usimamizi wa forodha na kodi ngazi zote kuanzia astashahada, stashahada na Shahada na shada ya uzamili kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo cha Muenster cha Ujerumani, katika sheria ya kodi na usimamizi.

Pia alisema mafunzo hutolewa ya muda mrefu na mfupi kwa taasisi mbalimbali pamoja na kufanya utafiti kuhusu masuala ya forodha na kodi ambayo husaidia nchi kutatua matatizo katika mifumo ya kodi.

# Tanzania, Ufaransa kukuza uchumi bluu

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imesema ushirikiano wa kibiashara kati ya Tanzania na Ufaransa, unatarajiwa kuwa na faida kubwa katika sekta mbalimbali nchini.

Miongoni mwa faida ni kutengeneza fursa za ajira na biashara, na utakaochochea kuongezeka kwa pato la taifa na kukuza uchumi wa bluu.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Leonard Chamuriho, alisema juzi katika semina iliyoandaliwa na Ubalozi wa Ufaransa jijini Dar es Salaam, na kuhudhuriwa na wafanyabiashara wa Ufaransa.

Alisema semina hiyo ilihusu majadiliano ya kukuza uchumi wa bluu, na ilifanyika nchini kutokana na uwapo wa maziwa pamoja na bahari ambazo zinatoa fursa nyingi za uwekezaji ambapo zikitumiwa vizuri, zitasaidia katika kufikia matarajio ya uchumi wa bluu.

"Tumekutana na makampuni ya Ufaransa nane pamoja na taasisi zetu sita ambazo zimekuja kujadili ushirikiano katika kupata na kuchangamkia fursa za uchumi wa bluu.

"Pia tumeongelea kuhusu masuala ya uvuvi hasa katika bahari ya ndani, pia tumeongelea suala la ujenzi wa meli na jinsi ya kutoa taka za meli katika maji, kutunza na kusafisha mazingira na jinsi ya kujua kuwa kuna uchafuzi wowote uliojitokeza katika maeneo hayo," alisema.

Aliongeza kuwa mambo mengine waliyojadiliana ni masuala ya ulinzi kwenye bahari hasa upande wa uvuvi, ambao ni miongoni mwa eneo lanalohusika katika kukuza uchumi wa bluu.

Aidha, alibainisha fursa zilizopo na kujadiliwa ukiwamo uchimbaji wa mafuta katika bahari pamoja na gesi, ambapo makampuni hayo yanaangalia fursa zote hizo na yamekuja kwa ajili ya kuongea na makampuni ya ndani ili kuangalia ni jinsi gani yanaweza kushirikiana katika kuchangamkia fursa hizo.

Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier, alisema watatunza na kukuza ushirikiano wao na Tanzania katika nyanja mbalimbali kwa dhumuni la kuchochea maendeleo na kukuza uchumi wa bluu.

"Kampuni mbalimbali Za Ufaransa zipo hapa kwa ajili ya kuimarisha ushirikiano kwa kuangalia na kuzifanyia kazi fursa zilizopo hasa katika sekta ya kilimo, uvuvi, usafirishaji, ulinzi, bandari na miundombinu, katika kukuza uchumi wa bluu.

"Hii italeta muunganiko na kutuweka pamoja na sekta mbalimbali na kufanya kazi kwa ushirikiano, jambo ambalo litaleta tija katika kukuza uchumi wa bluu," alisema.



Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omar Kumbilamoto (kushoto), akizindua kampeni ya usafi itakayoendeshwa na asasi ya Emmanuel Brotherhood Foundation (EBF) na inayofadhiliwa na Serikali ya Ujerumani kupitia shirika lake la GIZ, chini ya mradi wake wa DeveloPPP, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# DC akemea utendaji kazi kwa mazoea

**Na Zuhura Zukheir,** IRINGA

MKUU wa Wilaya ya Iringa, Mohammed Moyo, amekemea tabia ya baadhi ya watumishi na watendaji wa wilaya hiyo kufanya kazi kwa mazoea badala yake wafanye kazi kwa kuzingatia matokeo chanya.

Moyo alisema hayo juzi baada ya kukagua miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa huku akibainisha kwamba katika ziara yake amegundua watumishi wengi wanafanya kazi kwa mazoea katika maeneo yao.

Alisema watumishi wengi bado hawazingatii muda wa kwenda kuwatumikia wananchi kwa kuwa wamekuwa wanafanya kazi kwa muda ambao wanajitakia tofauti na ule uliopangwa.

Katika miradi mingi aliyoitembelea, alisema amegundua ucheleweshaji wa kukamilika kwa shughuli unatokana na watendaji wa serikali kutowasimamia vizuri makandarasi ambao wanakuwa wamepewa zabuni ya kufanya kazi husika.

Alisema wafanyakazi walioajiriwa na serikali wanapaswa kufanya kazi kwa weledi unaotakiwa na kuacha mara moja kufanya kazi kwa mazoea kama ilivyokuwa awali. "Hiki ni kitabu kingine, hivyo unatakiwa kufanya kazi kulingana na zama za kitabu husika ili kuendana na serikali ya awamu hiyo kwa lengo la kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambayo ndiyo imechangia kuwapo kwa serikali ya awamu ya sita," alisema .

Moyo alisema watumishi wote wanatakiwa kufanya kazi kwa umakini mkubwa ili kuhakikisha wanawatumikia wananchi kama inavyotakiwa kulingana na sheria za utumishi wa umma kwa lengo la kuleta maendeleo. Alisema kwenye mikutano yote watumishi na yeye mwenyewe wanatakiwa kufika kwa wakati na kuacha mara moja tabia ya kuwakalisha muda mrefu wananchi wakiwasubiri viongozi kufika na matokeo yake kuwapunguzia muda wa kufanya kazi za kujiletea maendeleo. Baadhi ya watendaji wa mitaa, vijiji na kata pamoja na maofisa tarafa wa Wilaya ya Iringa, waliahidi kutekeleza maagizo ya kiongozi huyo ili kuendana na kasi ya serikali katika kuwatumikia wananchi.

Naye Meya wa Manispaa ya Iringa, Ibrahim Ngwada, alisema atahakikisha anawasimamia watumishi wa halmashauri hiyo ili waache tabia ya kufanya kazi kwa matakwa.

# Tanzania yaishukuru Ujerumani kwa kudhamini kampeni usafi

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI ya Tanzania imeishukuru Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika lake la Maendeleo la GIZ chini ya mradi wake wa DeveloPPP kwa kudhamini kampeni ya elimu kuzuia magonjwa ya kuambukiza na kutoa bidhaa mbalimbali za usafi bure kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

Shukrani hizo zilitolewa jana Dar es Salaam na Meya wa Jiji, Omar Kumbilamoto, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya usafi itakayoendeshwa na taasisi ya Emmanuel Brotherhood Foundation (EBF) kwenye wilaya za mkoa wa Dar es Salaam.

Alisema walengwa kwenye kampeni hiyo ambayo itahusisha viongozi wa serikali za mitaa ni mama na baba lishe, wauzaji wa samaki, madereva wa daladala na makondakta wanaotarajiwa kuwa 25,000.

"Tunawashukuru sana GIZ na EBF kwa kutoa vifaa vya usafi, niwahakikishie kwamba mmeleta sehemu sahihi lakini naomba msiishie hapa Dar es Salaam nendeni mikoani nako mkafanye kampeni kama hii na mtoe sabuni za usafi kama mlivyofanya hapa," alisema Meya.

Alisema Jiji la Dar es Salaam halijapata milipuko ya magonjwa kwa muda mrefu kutokana na kampeni mbalimbali za kuweka mazingira katika hali ya usafi, hivyo kampeni hiyo imekuja wakati mwafaka kufanya usafi kuwa ajenda endelevu.

Mshauri wa EBF, Alex Benson, alisema kupitia mradi huo, vifaa vya usafi vitakavyotolewa bure ni ndoo na sabuni za kunawia mikono, dawa za kuua vijidudu, vitakasa mikono na taulo za kike zitawasaidia walengwa kufanya kazi katika mazingira safi.

Alisema nia ya mradi huo ni kuhakikisha mazingira yao ya biashara yanakuwa safi kutokana na ukweli kwamba magonjwa ya kuambukiza yanaweza kuzuilika kwa njia ya usafi na watu wakiwa na afya njema wanashiriki vizuri shughuli za uchumi.

Takwimu za miaka ya hivi karibuni zinaonyesha kuwa serikali imekuwa ikitumia takriban asilimia 70 ya bajeti ya afya kugharamia matibabu ya magonjwa ya kuambukiza yanayosababishwa na uchafu wa mazingira.

Alisema wadau wa mradi huo watatoa elimu na kuhamasisha utamaduni wa usafi katika jamii ili kulinda afya ya jamii kwa ujumla kwani magonjwa mengi yanazuilika kwa njia ya usafi.

Aliishukuru serikali kupitia wizara ya afya kwa kuidhinisha matumizi ya vipeperushi vyenye ujumbe mbalimbali na kusaidia kuratibu kampeni hiyo ambayo itawanufaisha Watanzania wengi.

"Kipekee tunaishukuru serikali ya Ujerumani kupitia shirika lake la GIZ kwa kuona umuhimu wa kufadhili kampeni hii ya usafi na kutumia kampuni za ndani kama Bingwa Laboratories Ltd na AFRICRAFT kutengeneza bidhaa zinazotumika katika kampeni hii, kwa pamoja tunasema magonjwa mengi yanazuilika kwa njia yaa usafi," alisema



# Wizara yajitosa hoja za mkaguzi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, imeanza kushughulikia hoja zilizoibuliwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa taasisi zake sita ili kuandaa vitabu vya hesabu na utekelezaji wa mapendekezo yaliyobainishwa.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Zainabu Chaula, aslisema hayo jana alipokuwa akifungua kikao kilichokutanisha taasisi hizo jijini hapa.

Alisema wameamua kukaa pamoja kwa kuwa mwaka jana walikuwa hawajafanya vizuri na kulikuwa na sintofahamu katika taasisi mbili.

"Kikao tulikipanga na ni cha mkakati kwa sababu masuala ya ukaguzi yapo kisheria, katika Taasisi sita zinapaswa pia kufuata sheria hizo, kazi ya kiongozi ni kuhakikisha kanuni, taratibu na sheria zinafuatwa, binadamu bila kumfuata kwa karibu tegemea kufeli," alisema.

"Katika taasisi wako waliofanya vizuri lakini wapo waliokuwa na hoja za kutosha, na kweli mara nyingi tunazitengeneza wenyewe kwa hiyo wao kama wahasibu wa ndani ambao tumewapa jicho la kwanza haya ni maandalizi ili CAG akija akute mambo yamekaa sawa sio kwa kutengeneza tunataka kutengeneza utamaduni huu," aliongeza.

Alisema wameamua kuweka utaratibu huo kwa sababu mara nyingi wanapokuja wakaguzi wanakuta baadhi ya vitu havipo sawa hivyo wanatengeneza utamaduni wa uwajibikaji wa pamoja.

"Tunatengeneza utamaduni wa uwajibikaji wa pamoja, kwa sababu mara nyingi wanapokuja wakaguzi wanakuta baadhi ya vitu havipo natamani kuna mambo mengine ni ya msingi lakini hatuyatekelezi sasa hapa nimekuja kuwaambia nini tunatarajia na wamekuja wahasibu na wakaguzi wa ndani wao ndio wanapaswa kuwasaidia," alisema.

Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Wizara hiyo, Joyce Christopher, alisema wapo kwa ajili ya kikao kazi ambapo taasisi sita zimejumuika wakiwamo wakaguzi wa ndani na wahasibu. Lengo ni kupanga mipango ya pamoja jinsi ya kufunga mwaka na utekelezaji wa hoja zilizoibuliwa na CAG.

"Majukumu ya kitengo cha ndani katika kuhakikisha hoja za CAG zinafanyiwa kazi lengo ni kuboresha na kuhakikisha tunafanya vizuri pia kuangalia thamani ya fedha za serikali zinaonekana," alisema.

# Ndugai ataka TANESCO Mkoa wa Kongwa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameliomba Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuanzisha mkoa wa kishirika Kongwa ili kusogeza huduma karibu na wananchi.

Ndugai alitoa ombi hilo kwa Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, wakati wa ziara yake ya kukagua miradi ya umeme wilayani hapa.

"Mheshimiwa Waziri kutokana eneo hili hapa Mbande Wilaya ya Kongwa kuwa karibu na wilaya kubwa na miji midogo midogo mingi, tunaomba serikali kuanzisha Mkoa wa ki-TANESCO ili kusogeza huduma karibu na wananchi wa maeneo ya upande huu," alisema.

Ndugai alisema kufunguliwa kwa ofisi hiyo kutasaidia kusongeza huduma karibu na wananchi wa Wilaya za Kiteto, Mpwapwa, Gairo na Kongwa.

Alibainisha kuwa kwenye wilaya hizo kuna miji midogo mikubwa ambayo inakuwa kwa kasi na inahitaji huduma za umeme hivyo kutegemea Dodoma mjini inachelewesha huduma.

"Tunashukuru serikali kuwa na mpango wa kujenga kituo cha kupoza umeme kwenye wilaya yetu ya Kongwa, basi uwapo wa kituo hicho uendane sambamba na kuanzishwa kwa mkoa wa ki-TANESCO," alisema.

Aliongeza kuwa Wilaya ya Kongwa ni iko katikati na karibu na wilaya zingine alizotaja hapo juu, hivyo itarahisisha kuyafikia maeneo yote.

Aidha, alisema maeneo hayo yamekuwa yakikabiliwa na tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara, hivyo kuanzishwa kwa mkoa huo wa ki- utasaidia kuhudumia kwa wakati.

Waziri wa Nishati, Dk. Kalemani, alisema serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan ni sikivu, hivyo italifanyia kazi haraka ili kuondoa kero hiyo.

Dk. Kalemani alisema hilo linawezekana kwa sababu lengo ni kurahisisha huduma na kuwa karibu na wananchi hivyo utekelezaji unawekana.

"Kwa kuwa tuna eneo kubwa la kujenga mradi wa kupoza umeme hapa Wilaya ya Kongwa katika kijiji cha Machenje, naona kama ndio itakuwa mkoa tayari,"alisema.

Alisema serikali imetenga Sh. bilioni 41.2 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kupoza umeme kwenye Kijiji cha Machenje utakaoondoa tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara.




Mkurugenzi wa kiwanda cha kukamua mafuta ya alizeti cha Mwaja Mills, Mohamed Mwaja, akitoa kero yake kwa Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (hayupo pichani), kuhusu kukatika kwa umeme mara kwa mara kwenye mji mdogo wa Kibaigwa, Wilayani Kongwa, mkoani Dodoma mapema wiki hii. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Shirika lajitosa utapiamlo, udumavu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA lisilo la kiserikali la World Vision, limejipanga kutoa elimu kwa wanawake wa Mkoa wa Dodoma kuhusu unyonyeshaji ili kusaidia kuondokana na tatizo la utapiamlo na udumavu.

Meneja wa Mradi wa Lishe wa Mama na Mtoto, unaotekelezwa katika wilaya za Chemba na Bahi mkoani Dodoma, Daudi Gambo, alisema hayo wakati akizungumzia maandalizi ya Wiki ya Unyonyeshaji itakayofanyika Agosti Mosi hadi 7, mwaka huu.

Gambo alisema lengo la kufanya hivyo ni pamoja na kutoa elimu juu ya unyonyeshaji kwa watoto wadogo lakini pia namna ya kuandaa lishe bora ya watoto ili kupunguza upungufu wa uzito na vifo.

"Tunatarajia kutoa elimu kwa wajawazito katika wiki ya unyonyeshaji ambayo itaanza wiki ijayo katika wilaya ambazo mradi unatekelezwa. Lengo ni kutaka wajue majukumu yao katika unyonyeshaji," alisema Gambo.

Alisema wamekuwa wakiwaelekeza namna ya kutengeneza lishe bora kwa watoto na wamekuwa wakifundishwa mafungu matano ya vyakula ambayo yanatakiwa kwamtoto na kuwasisitiza kunyonyesha kwa muda wa miezi sita.

Hata hivyo, alisema elimu hiyo imekuwa ikiwasaidia kinamama wenye watoto wadogo na mahudhurio mazuri kliniki.

Pia alisema wamekuwa wakitoa vifaa vya hospitali kwa ajili ya matumizi mbalimbali vikiwamo vya kuchemshia vifaa vilivyotumika kuhudumia wagonjwa, vifaa vya kupimia wingi wa damu, vitanda vya kuzalia, mashine ya kupimia shinikizo la damu na kifaa cha kupima maendeleo ya mgonjwa.

Aliwasisitiza wananchi kuzingatia elimu wanayopewa na wataalamu wa afya ili kusaidia kuwafundisha jinsi ya kuwalea watoto wao.





# Zanzibar yarasimisha bajaji na bodaboda

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imerasimisha usafiri wa bajaji na bodaboda na kuweka kanuni na masharti maalum katika biashara hiyo.

Akizungumza na waandsihi wa habari jana, Mkurugenzi wa Usafiri na Leseni Zanzibar, Muhammed Simba Hassan, alisema serikali imechukua uamuzi huo kutokana na vijana kujiajiri katika usafiri huo. Alisema usafiri huo utasajiliwa kwa ajili ya biashara ya kusafirisha abiria na kuwa na namba maalum za usajili.

Simba alisema madereva wa vyombo hivyo watapewa elimu ili kufuata sheria za usalama barabarani na kuepukana na ajali zisizo za lazima.

Kuhusu nauli katika usafiri huo, Simba, alisema itakua ni makubaliano kati na mtoa huduma lakini wakigundua kama kutakua na malalamiko kuhusu nauli itabidi waweke kiwango maalum

Naye Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Rahma Kassim Ali, alisema usafiri huo unaendelea kukua kwa kasi na kwa vijana ni sehemu yao ya ajira katika kujipatia kipato.

Alisema urasimishwaji huo umekuja kwa mujibu wa uwezo aliopewa chini ya kifungu cha 48 (4) cha Sheria ya Usafiri Barabarani Na. 7 ya Mwaka 2003.

Waziri huyo aliwataka wananchi wanaotaka kuingia katika biashara hiyo kufika katika mamlaka husika ili kupatiwa utaratibu wa kupata leseni ya biashara hiyo.

Pia aliwataka wananchi wanaotumia usafiri huo kuwa waangalifu na kuhakikisha wanapanda katika vyombo vilivyosajiliwa ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani, Haji Ali Zubeir, akizungumzia utambulisho wa bodaboda hiyo, alisema huduma hiyo itatofautiana na vyombo vinavyosafirisha abiria wa kawaida kwa kuwa vyombo hivyo vitakuwa na usajili maalum.

Pia alisema waendesha bodaboda na bajaji watakuwa na mavazi maalum yanayowatambulisha kuwa wanafanya biashara hiyo na watapangiwa vituo maalum kwa ajili ya kupakia abiria.

"Hadi tunatoa taarifa hii ya urasimishaji wa usafiri huyo tayari tumeshasajili vyombo 13,000 zikiwamo bajaji na bodaboda," alisema.

Muhammed Mahmoud Hassan, Mtunza Hazina wa Jumuiya ya Bodaboda Zanzibar, ambaye pia ni dereva wa usafiri huo katika kituo cha Hospitali na Mnazi Mmoja, aliipongeza serikali kwa hatua hiyo kwa sababu ni kilio chao cha muda mrefu kutaka urasimishaji wa biashara hiyo.

"Tumefurahi sana kuwa biashara hii sasa ni rasmi, cha msingi kujielewa na kufuata masharti ili kuepuka kufanya makosa" alisema.

Alisema kurasimishwa kwa biashara hiyo na kuwekewa kanuni maalum, kutasaidia kupunguza malalamiko ya kuwa wafanyabiashara hao kujihusisha na matukio ya kihalifu ikiwamo udhalilishaji wa kijinsia na uporaji.

Madereva wanatakiwa kuelewa kuwa kazi hiyo ni kama kazi zingine na wananchi wahakikishe wanatumia usafiri huo kwa watu wanaowatambua ambao watakua na utambulisho maalum.

Yasir Nassor, dereva wa bodaboda katika kituo cha Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, alisema urasimishaji wa usafiri huo utapunguza changamoto zilizokuwa zikiwakabili na kuahidi kuendelea kufuata miongozo iliyowekwa.




Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Dk. Edward Hoseah, akitoa mada kuhusu Maadili ya Uongozi kwa wakurugenzi na wakurugenzi wasaidizi wa Ofisi ya Bunge, katika mafunzo yanayofanyika katika Ofisi Ndogo ya Bunge Zanzibar jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

## Miundombinu kujengwa kuzuia uharibifu wa kingo za bahari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya Salum, amesema serikali imeweka mkakati ya kujenga miundombinu ya kuzuia uharibifu katika fukwe za bahari zilizoathiriwa na mabadiliko ya tabia nchi.

Akizungumza na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Libereta Mulamula, alipofika na ujumbe wake ofisini kwake, Migombani mjini Unguja, alisema miundombinu hiyo ni pamoja na ujenzi wa kuta ambazo zitasaidia kuzuia mmomonyoko wa ardhi.

Alisema mmomonyoko wa ardhi unasababishwa na kupanda kwa kina cha maji ya bahari na matokeo yake kupotea kwa fukwe za bahari na baadhi ya visiwa vidogo vilivyozungukwa na bahari.

Pia alisema hatua hiyo imetokana na mabadiliko ya tabia nchi inayotokana na shughuli za kibinadamu zinazofanywa na wananchi wanaoishi karibu au kutumia fukwe hizo.

Alisema kwa sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Idara ya Mazingira, imeanza kujenga ukuta katika Bahari ya Kijiji cha Msuka Wilaya ya Micheweni, Pemba ili kuzuia uharibifu wa fukwe hizo.

Naye Balozi Mulamula alisema ushirikiano uliopo baina ya ofisi hizo utazidi kuimarishwa katika kupambana na mabadiliko ya tabia nchi.

Aliipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa hatua inazochukua katika kutokomeza uuzaji na matumizi ya dawa za kulevya sambasamba na matibabu wanayopatiwa waathirika wa dawa hizo.

Mulamula aliahidi viongozi wa wizara yake kufanya kazi kwa ushirikiano na ofisi hiyo ikiwa ni pamoja na kufanya ziara za mara kwa mara ili kufika Zanzibar na kujifunza utunzaji wa mazingira.

# SMZ yasisitiza nafasi ya wafanyabiashara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatambua na kuthamini mchango wa wafanyabiashara katika kuunga mkono ujenzi wa miundombinu.

Alitoa kauli hiyo jana alipokutana na baadhi ya wafanyabiashara waliopo Zanzibar katika kujadili namna bora ya kuipatia ufumbuzi changamoto ya upatikanaji wa maji safi na salama Zanzibar kupitia kikao maalum kilichofanyika ofisini kwake, Vuga mjini Zanzibar.

Hemed aliwapongeza wafanyabiashara hao kwa kuitikia wito wa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa kujitolea katika masuala mbalimbali ya kimaendeleo ili kupunguza changamoto zinazowakabili wananchi. Alisema mchango wao una umuhimu mkubwa katika kuijenga Zanzibar mpya na kueleza kuwa Zanzibar itajengwa na Wazanzibari wenyewe, hivyo hakuna haja ya kusubiri watu kutoka nje.

Hemed alisema serikali inatambua mchango wa wafanyabiashara wa ngazi zote na kwamba serikali ya awamu ya nane itatoa kila aina ya ushirikiano ili kuhakikisha mchango wao unaisaidia jamii moja kwa moja.

Aidha, alisema maeneo mengi ya Zanzibar bado yanakabiliwa na ukosefu wa maji jambo ambalo limesababisha kuwashirikisha wafanyabiashara ili kujadili kwa pamoja na kutoa mawazo kwa lengo la kuitatua changamoto hiyo.

Akizungumzia umuhimu wa maji safi na salama, Hemed alisema huduma hiyo ni ya muhimu katika maisha ya kila siku ya binadamu, hivyo ni vyema kukawekwa mazingira mazuri ili kupatikana kwa urahisi.

Naye Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Suleiman Masoud Makame, aliwashukuru wafanyabiashara hao kwa kuitikia wito huo na kwa kukubali kuunga mkono jitihada hizo ili kuisaidia jamii kuondokana na tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama.

Alisema Mamlaka ya Maji Zanzibar imebadili mfumo wa ukusanyaji wa mapato na kwa sasa ina mfumo mzuri ambao utawasadia kupata fedha za kuendeshea mamlaka hiyo kutokana na makusanyo yatakayopatikana.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar, Dk. Salha Muhammed Kassim, alisema kwa sasa wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa vyanzo vya maji, upungufu wa pampu ambapo kwa sasa kunahitajika jumla ya pampu 41.





## DUNIA YA ZUCHU

# Nandy, Anjella wanaing'arisha

WANAMUZIKI nyota wa kike, Zuchu, anazidi kuonyesha kwamba ameingia katika sanaa ya muziki si kwa bahati mbaya, bali amedhamiria kufanya maajabu.

Awali soko la muziki kwa upande wa wanawake lilitawaliwa na Nandy, ambaye aliawateka mashabiki na kuonekana hakuna atakayeweza kumshika.

Wakati Zuchu ameibuliwa na lebo ya WBC, upande wa lebo ya Konde Gang, wakamtengeneza Anjellah kuwa mshindani katika mbio hizo za muziki.

Pamoja na ushindano huo, Zuchu anaonekana kutoshikika na kupasua mawingu kutokana na kutoa nyimbo tamu na zenye utofauti mkubwa na wenzake.

Kutokana na kupata umaarufu kila kukicha, msanii huyo amekuwa na kipato kikubwa kuliko wasanii wenzake kutokana na kupata dili nono za kibiashara, matamasha na malipo yanayotokana na mtandao wa You Tube.

Kwa mfano mtandao wa You Tube, imemlipa kiasi cha Sh. milioni 10, ndani ya mwezi mmoja kupitia chaneli yake na anaweza kuongeza kiwango cha pesa endapo ataendelea kuwapagawisha mashabiki wake.

Licha ya Nandy, kuamua kupambana kwa nguvu hasa kwa kuandaa matamasha yake mwenyewe, lakini bado ameachwa mbali.

Zuchu ambaye anatamba kwa sasa na wimbi wa "Nyumba Ndogo" ameonekana kuwa kama alama kwa vijana wa kike wanaoweza kufanikiwa kwa kufuata ndoto zao, hata kama ikichelewa.


BASI SAWA

## Steve RnB umeanza kuwananga wenzio



MWANAMUZIKI wa Bongofleva, Steve RnB amewataja wasanii wenzake Jux na Ben Pol, kuwa ni waoga kujitambulisha kama waumini wa muziki wa RnB.
Steve RnB pamoja na wasanii hao kutaja kwamba ni wakongwe wa muziki wa aina hiyo, yeye anaona hawakustahili kupewa sifa hizo.
"Kwenye RnB huwezi kutaja bila kuweka jina la Steve, hata hao uliowataja hawawezi kuwa nguvu kama hiyo kwa kutaja RnB mbele ya majina yao, sijajiita Steve RnB bali mashabiki ndio wamenipa," amesema.

## Stamina kwani umetumwa kumtetea?



RAPA mkali hapa Bongofleva, Stamina Shorwebwenzi, amemkingia kifua mwanamuziki mwenzake Shetta, akimtaja kama mtu mwenye bidii na hawezi kuwa katika kundi la uchawa.
"Shetta ni mjanja mjanja sana, kati ya miamba ambayo naiaminia yeye kiboko, anajua kuitafuta fursa na haiachi, ule ndio unyama na inavyotakiwa, watu wengi wanamweka kwenye kundi la uchawa kwangu mimi simuoni " amesema Stamina
Ameeleza kuna baadhi ya vitu Shetta anavifanya ambavyo yeye hawezi hata kuvigusa.



## Rhino atua Bongo kuwafuata mastaa

MSANII wa kizazi kipya mwenye makazi yake nchini Marekani, Rhino The Don, ametua nchini kukamilisha kolabo zake kadhaa na mastaa mbalimbali wa muziki.
Rhino The Don ambaye licha ya kuishi Marekani amekuwa akifanya kazi na wasanii wa Tanzania huku nyimbo zake zikipata mafanikio makubwa kwenye mitandao ya kijamii.
Akizungumza na BT, Rhino The Don amesema baada ya kufanya kolabo na mastaa wakubwa kama Shetta na Mr Blue, amekuja Tanzania kikazi zaidi kwani kuna nyimbo kadhaa amekuja kuzikamilisha.
"Nimekuja kikazi zaidi kuna ngoma nimefanya na wasanii wakubwa wa hapa lakini pia mimi ni mwekezaji kwahiyo nimekuja kuwekeza na mambo mengine kama hayo, nitakuwepo hapa Tanzania kwa muda kufanya hayo mambo kadhaa," amesema mkali huyo kutoka Utah, Marekani



## Neva: Wema hao, wabaya ni hao hao

**Na Adam Fungamwango**

DUNIANI hapa unaweza kupata matatizo hadi ukakufuru Mungu. Halafu matatizo yenyewe yanasababishwa na binadamu pia. Cha muhimu ni kumuomba Mungu akuepushie na balaa. Kwa sababu watakaokuja kukusaidia na kukuokoa ni hao hao binadamu.

Binadamu mmoja anaweza kukufanya uwe na matatizo, lakini ukakutana na mwingine atakusaidia.

Leo tutaiangalia filamu ya 'Neva', ambayo inamhusu msichana mmoja mwenye jina hilo la Neva, alipoingia kwenye matatizo ambayo yamesababishwa na binadamu na kumfanya maisha yake yawe ya shida.

Filamu imechezwa na Barton Richard, Eshe Mohamed, Joyce Temu, Mzee Jengua, Ibrahim Kitimbu, Asha Rajab na wengineo.

Kijana Bizo anapita sehemu ya kuuzia chakula na kumkuta mama mmoja akimkoromea msichana ambaye ana mtoto mgongoni.

Kuuliza anaambiwa kuwa aliomba kibarua cha kuosha vyombo ili apate ujira wa ukoko.

Bizo anatuliza hali hiyo kwa kumnunulia chakula msichana huyo. Anaahidi kumsaidia zaidi.

Bizo anakwenda kuangalia sehemu anayoishi msichana huyo, lakini hairidhishi.

Neva akamwambia alifukuzwa nyumbani kwao na wazazi kutokana na kupata mimba akiwa shuleni.

Katika kuulizana maswali, Bizo anamkumbuka msichana huyo. Bizo ni daktari kwenye hospitali moja.

Anamwambia alishawahi kuletwa akiwa amebakwa na zaidi ya mwanamume mmoja na aliletwa hospitalini akiwa hajitambui.

Na cha zaidi alikuwa tayari ameshaambukizwa gonjwa la UKIMWI. Na mtu aliyemleta hospitali ana anaitwa Bravo.

Bizo alipoondoka, anakuja msichana mmoja kwa Neva na kumwambia anafahamu yaliyomkuta kwa sababu ameambiwa na Bravo.

Ni kwamba Bravo alimwambia msichana Mona kuwa alimwekea dawa Neva, akambaka na akawaita rafiki zake wakambaka pia. Kisa eti alimsumbua sana.

Neva anakwenda nyumbani kwa dokta na kuomba amuche mtoto wake kwani anakwenda sokoni.

Daktari Bizo anampa laki moja kwa ajili ya kufanya 'shopping'. Neva hafanyi hivyo, analipiza kisasi kwa kuwaua wote waliombaka.

Anafungwa jela na kutoka kwa msamaha wa rais baada ya mwaka mmoja.





## Bonge la Nyau hizo sasa sifa

MSANII wa BongoFleva, Bonge la Nyau, amejinasibu kuwa rangi yake ya mchanganyiko imekuwa kama kero kutokana na wanawake kumsumbua kimapenzi.
Bonge la Nyau amesema hata watu wenye rangi kama yake wanakabiliana na hali hiyo ambayo inawafanya kuwa makini wasije wakaangukia katika mikono mibaya.
"Kila binadamu ana mawazo kuhusu wanawake, si unajua mashombeshombe kama sisi tunasumbuliwa na wanawake, sioni kama wanawake wanaweza kunifanya akae kimya kwenye muziki" amesema Bonge la Nyau.

## Masongi ya kihindi yaliyotesa Uswazi

**Na Adam Fungamwango**

KWA wale vijana au watoto katikati ya miaka ya 1980 hadi katikati ya miaka ya 1990, wanakumbuka jinsi kulivyokuwa na filamu nyingi kali za kihindi.

Achilia mbali kile kizazi cha mwanzoni mwa miaka ya 1980, kilichokuwa kikienda Drive Inn Cinema, Odeon, Avalon, ambapo mitaani hakukuwa na video wala televisheni, kulikuja kizazi kingine ambacho tayari video angalu moja moja zilianza kuonekana mitaani.

Badala ya watoto kwenda kwenye majumba ya sinema na ilikuwa kwao ni ngumu kidogo, sasa walianza kwenda kwenye nyumba za watu ambao walikuwa wakionyesha filamu mbalimbali.

Kila mkoa nchini Tanzania kulikuwa na sehemu ambazo watoto walikuwa wakienda filamu.

Dar es Salaam hasa maeneo ya Kinondoni kulikuwa na sehemu maarufi kama 'Milano' na 'Morocco', karibu kabisa na Kanisa Katoliki Magomeni.

Kwenye filamu za Kihindi, mbali na utamu wa filamu zenyewe, lakini vijana na watoto walipenda sana nyimbo zake.

Baadhi ya nyimbo za Kihindi zikawa maarufu sana mtaani na wala haikuwa ajabu kukuta zikiibwa vijana na watoto. Wenyewe wakazibatiza jina na kuyaita 'masongi'. Walikuwa na maana ya nyimbo kwa lugha ya kizungu 'songs'.

Hapa leo tutaziangalia baadhi ya masongi ya Kihindi yaliyotamba na kupendwa sana enzi hizo.

### Goron Ki na Kalon Ki

Ni moja kati ya 'songi' maarufu sana kwa vijana na watoto wa miaka ile ya 1980 hadi 1990. Sidhani kama kuna aliyekuwa mtoto au kijana licha ya kwamba sasa atakuwa mtu mzima, asiufahamu.

'Goron Ki na Kalon Ki' ni wimbo ambao upo kwenye filamu ya 'Disco Dancer' ambayo staa wa picha alikuwa ni Mithun Chakraborty.

Filamu hii maarufu sana na iliyotokea kupendwa ilitoka mwaka 1882, na ilikuwa na 'masongi' mengi makali 'Goron Ki na Kalon Ki, Duniya Hai Dilwalon Ki.' Hiyo ni sehemu ya wimbo huo.

### Jimmy Jimmy aaja

Hapa sasa ndiyo balaa. Hili 'songi' la Jimmy, ukikuta watoto mtaani wanaliimba utafurahi na roho yako.

Halafu kila mmoja anaujua wimbo huu kikamilifu kwa sababu ni sehemu ambapo staa wa picha Mithun anakwenda kushika gitaa lililotegwa umeme, mama yake atakuja kumuokoa. Filamu ni hiyo hiyo Disco Dancer.

### Juma Chuma Dede

Mwaka 1991 kulitoka filamu moja kali ya Kihindi iliitwayo 'Hum'. 'Starlingi' wake ni Amitabh Bachchan.

'Juma Chuma Dede' ni moja kati ya 'songi' lililopendwa sana na mashabiki wengi wa picha za kidosi au filamu za Kihindi wakati huo. Na hata hapa nchini bendi ya Varda Arts imeshawahi kuchukua mirindimo ya wimbo huo na kuimba kwa kiswahili.

### Kuch Kuch Hota Hai

'Songi' hili kali lipo kwenye kwenye filamu kali ambayo inaenda kwa jina hilo hilo. Ilitoka mwaka 1998 na kuushtua ulimwengu wa filamu za Kihindi duniani. Staa wa picha hiyo ni Shah Rukh Khan, huku wimbo huo ikitia fora na kupendwa na watu wengi zaidi kuliko wimbo wowote ule kwenye picha hilo.

### My Tarzan

Tarzan ni moja kati ya filamu maarufu mno nchini Tanzania na duniani kote. Ilikuwa ni filamu iliyoonyesha kuwa mapenzi yanaweza kumea popote pale hata pasipo na mbolea, porini na kwa mtu yoyote yule. Ndani yake kuna 'masongi' kibao mazuri, lakini uliokuwa rahisi zaidi kuimbwa na Wabongo uliitwa 'My Tarzan', ambao ulifunika bovu.



# Big Brother Naija yaanza kurindima



MASHABIKI na wapenzi wa shindano la maisha halisi la Big Brother Naija (BBN) wameanza kufurahia msimu wa sita wakitarajia kuona burudani ya aina yake.

Jumla ya washiriki 22 wataishi katika jumba moja, kati ya hao wanawake 11 na idadi kama hiyo ni wanaume ambao wote kwa pamoja watawania kitita cha Sh. milioni 500, kwa mshindi wa kwanza.

Mwaka jana shindano hilo halikufanyika kutokana na sababu mbalimbalia ikiwamo ugonjwa wa virusi vya Corona pamoja na malalamiko kutoka kwa baadhi ya watu kwamba kuna vitendo vinavyofanyika vinakuwa kinyume na maadili.



## Paris fahamu tumbo halifichwi

MREMBO bilionea mwenye wafuasi wengi katika mitandao ya kijamii, Paris Hilton, amekana taarifa zilizosambaa kwamba ana ujauzito wa mtoto wake wa kwanza.

Paris ambaye ana utajiri wa kutisha, amesema habari hizo si za kweli kwani hatarajii kupata mtoto hivi karibuni na hivyo hana ujauzito.

"Nimesoma ujumbe zaidi ya tatu ,katika simu yangu ya iPhone, kila mtu akinitakia Baraka na kunipongeza, najisikia furaha kwangu lakini sitarajii kupata mtoto kwa sasa," ameandika kupitia akaunti yake ya Instagram.

## Georgina unachosema kina mashiko

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Georgina Onuocha, amewashauri wanawake wenzake kufanya kazi kwa bidii na kuacha tabia ya kuwategemea wanaume kwa kila kitu.

Nyota huyo wa filamu ametoa ushauri huo baada ya kufanikiwa kumaliza shahada yake ya kwanza, ambapo aliambatanisha na picha kadhaa akionekana akitunukiwa cheti.

Georgina alisema wakati wa mwanamke kulala au kuacha kazi kwa kumtegemea mwanamume umekwisha, kwani kila mtu anatakiwa kufikia malengo yake kwa wakati.





## Issa Rae harusi haina siri

MSANII wa filamu wa Marekani, Issa Rae, ameripotiwa kufunga ndoa kwa siri na mchumba wake Louis Diame.

Mashabiki wa msanii huyo walishtushwa na picha zilizotoka siku ya Jumatatu zikimwonyesha akiwa katika vazi la harusi na mkewe huyo.

Hata hivyo, taarifa zinasema sherehe ya harusi hiyo ilifanyika kwa siri na kuwahusisha ndugu na jamaa wa karibu pekee.

## Sonia hukujua kuna marafiki na viatu?

ALIYEKUWA mke wa mwanasoka maarufu wa Nigeria, Sonia Ighalo , amemshutumu mshiriki wa zamani wa shindano la Big Brother Naija, Uriel kuwa ana uhusiano kimapenzi na mume wake.

Sonia kupitia ukurasa wake wa Instagram, amesema Uriel alilala na mume wake Odion Ighalo, huku akiweka wazi kwamba ushahidi wa ujumbe wa simu alizokuwa wakiwasiliana anao.

"Kwa nini mwanamke anatamani mali ya mwanamke mwenzake? Naweka picha ambazo mume wangu wa zamani alikuwa akifanya na rafiki yangu wa karibu ni mambo machafu kuyaona," ameandika.



MAKALA

# Ongezeko la wagonjwa wa vidonda vya tumbo linapohatarisha ustawi wa afya katika jamii

**Na Christina Mwakangale**

VIDONDA vya tumbo au kitaalam vinafahamika kama 'ulcers' au 'gastritis' ni miongoni mwa magonjwa ya mfumo wa mmeng'enyo wa chakula katika mwili wa binadamu unaoongezeka kwa kasi.


Matatizo ya vidonda vya tumbo huwasumbua watu wengi duniani na huwapata sana watu wazima kuliko watoto wadogo. Ugonjwa huu unatokana na uwepo vya kidonda katika baadhi ya sehemu ya utumbo kwenye mfuko wa kupokea chakula, utumbo mwembamba au mpana.


Daktari Jimmy Minja akizungumzia ugonjwa huo kwenye moja ya kituo cha televisheni nchini, anasema ugonjwa huo hutokana na sababu nyingi ingawa kwa nchi zinazoendelea chanzo kikubwa ni bacteria anayejulikana kwa jina la Helicobacter pylori (H. pylori).

Anasema asilimia zaidi ya 80 ya wanaougua vidonda vya tumbo hutokana na bacteria huyo, na kwamba wengi wanaougua ni walio na umri wa ujana kuanzia miaka 30 na 40, huku watoto na wazee idadi yao ya kupata maradhi hayo ni ndogo.

"Vidonda vya tumbo ni shida ambayo anaipata mtu kutokana na sababu moja au mbili ama nyingi, mara nyingi husababishwa na bacteria H. pylori, vidonda huwa katika mfuko wa chakula, sehemu ya kwanza ya utumbo mdogo au mkubwa," anasema Dk. Minja.

Anasema wapo watu ambao wanaishi na bacteria H. pylori maishani mwao na bila kupata tatizo kwa kuwa ni kati ya bacteria ambao huishi mwilini kama viumbe hai.



Dk Minja anasema bacteria wa H. pylori haambukizi kwa njia ya kugusana, bali husambaa kwa njia ya chakula au mate na kwenda kuathiri katika mfumo wa chakula.

**SABABU VIDONDA**

Dk. Minja anasema sababu nyingine ya vidonda vya tumbo mbali na bacteria, baadhi husababishwa na matumizi ya dawa za kutuliza maumivu muda mrefu bila kuzingatia ushauri wa kitabibu.

"Tumbo lina mfumo wake wa kujikinga tumboni kutokana na acid inayozalishwa, ili utumbo usiathiriwe kuna utelezi tumboni ambao huitwa 'mucus' ukinywa hizo dawa katika mchakato wake zinazuia 'mucus' kufanya kazi yake," anasema Dk. Minja.

Kuhusu imani tofauti zilizopo kwenye jamii namna ugonjwa huo ulivyo na chanzo kikitajwa kuwa ni kukaa njaa muda mrefu, kula vyakula vinavyozalisha acid nyingi, msongo wa mawazo, anasema dhana hizo si za kweli kwa sababu wengi hupata vidonda vya tumbo kutokana na bacteria H. pylori.

Msongo wa mawazo kwa aliye na vidonda vya tumbo, vitamzidia iwapo akiwa na hali hiyo,

**AINA ZAKE**

Aidha, Dk. Minja anasema aina ya kwanza ni vidonda vya utumbo mkubwa 'Gastric ulcers' ambavyo ni vidonda vya tumbo vinavyotokea ndani kwenye utumbo mkubwa. Pili ni vya utumbo mdogo 'Duodenal ulcers' ambavyo hutokea kwenye utumbo mdogo, hasa sehemu ya juu.

Anasema kwamba aina kwanza vinavyowakumba watu wengi, hutokea sehemu ya mwanzo ya utumbo mdogo akisema kati ya watu 10, sita wana vidonda aina hii.

Pili, anasema aina ya pili ambayo huwakumba zaidi wanawake ni vilivyopo kwenye mfuko wa chakula na kwamba aina hii maumivu yake huwa tofauti na kwa wanaougua maumivu huwa makali zaidi wakati wa kula chakula na yatapoa wakati chakula kikishashuka kwenye utumbo mkubwa.

"Maumivu ya aina ya vidonda vya tumbo huofautiana mengine huzidishwa na aina ya chakula, aina nyingine maumivu yatazidishwa unapohisi njaa, au baada ya kula," anasema Dk. Minja.

**DALILI**

Dk. Minja anasema dalili ya vidonda vya tumbo ni maumivu chini ya kifua 'gastric pain' na nyuma ya mgongo chini ya bega hii ikitokana na aina vidonda alivyonavyo mgonjwa.

"Dalili nyingine, kichefuchefu, gesi tumboni, upungufu wa damu mwilini, kutapika, ulaji mdogo wa chakula na kupungua uzito, anayepata shida baada ya kula mgonjwa ataona bora akae njaa kuliko shida anayoipata baada ya kula," anasema Dk. Minja.

"Nyingine ni kifua kuwaka moto, kupata pumzi ndogo, choo chenye rangi nyeusi kwa kuwa damu inakuwa inavuja katika vidonda na kutoka kupitia haja kubwa. Visipotibiwa huweza kusababisha kifo." Anaeleza.

Pia dalili nyingine ni kutapika damu, maumivu ya mgongo na misuli, kichomi, maumivu ya kichwa na kushindwa kula baadhi ya vyakula.

Pia, mara nyingi vidonda vya tumbo vinaambatana na chembe ya moyo yaani tumbo linaposumbua huuma kwa kuambatana na chembe ya moyo, mgonjwa huteseka kwa sababu anapangiwa chakula ambacho awe anakula na akila chakula tofauti hupata maumivu makali.

**TIBA**

Dk. Minja anasema vidonda vya tumbo baada ya kufanyiwa uchunguzi na kubainika bacteria huyo, matibabu huanza na kwamba tiba ikifuatwa ipasavyo hupona kabisa.

"Vidonda vya tumbo vina tiba iwapo kitaalamu imebainika, ila inashauriwa mtu mwenye vidonda vya tumbo kutokunywa pombe sababu acid ya tumboni huongezeka hata sigara hazifai," anasema Dk. Minja.

Anasema visipotibiwa ipasavyo huleta usumbufu wa mara kwa mara na baadhi ya jamii kudhani kwamba havina tiba huku baadhi wakitibu kienyeji.

# Siku ya Wanawake wa Afrika iwe chachu mapinduzi ya fikra, uchumi



Na Mwandishi Wetu

WANAWAKE wa ki- Afrika waliungana Julai 31, 1962 kabla ya serikali huru za Afrika kuunda umoja wao uliojulikana kama Umoja wa Nchi Huru za Afrika (sasa Umoja wa Afrika- AU) Mei 25, 1963.

Leo imetimia miaka 59 tangu Mkutano wa Kwanza wa Wanawake wa Kiafrika ufanyike Julai 27-31, 1962 Barani Afrika. Wanawake kutoka nchi huru 14 na vyama vinane vya ukombozi, walikutana katika Ukumbi wa Karimjee, Dar es Salaam, Tanganyika wakati huo. Vyama hivyo vilitoka Msumbiji, Angola, Zimbabwe, Namibia, Afrika Kusini, Guinea Bissau na Cape Verde.

Umoja wa Umajumui wa Wanawake Afrika (PAWO) ulizaliwa wakati Bara la Afrika likiwa chini ya utawala wa kikoloni. Wanawake waliamua kumkata jongoo kwa meno ili wawe bega kwa bega na wanaume katika kuikomboa Afrika.

Julai 31, 1962 walipuliza baragumu la kudai haki na ushiriki sawa na mapambano yaendelee hadi ushindi kamili. Lengo lilikuwa kujenga taifa la Afrika lenye waafrika wanaojiamini, wanaojitegemea kifikra, kiuchumi na kijamii na waendelee kutoa mchango wao duniani katika medani za sanaa, sayansi na teknolojia.

Leo siku hiyo inaadhimishwa na wanawake wa Kiafrika pote duniani. Baadhi ya nchi za Kiafrika zinaitambua siku hii maalum si tu kwa heshima ya wanawake na wasichana kama walezi wa taifa, bali pia ni siku ya uchechemuzi na kuchagiza ari waliyokuwa nayo waasisi ya kuendelea kudai uhuru, haki na usawa, amani na maendeleo kwa wote.

Baada ya marais Kwame Nkrumah (Ghana), Sekou Toure (Guinea), Modibo Keita (Mali) na Mwalimu Julius Nyerere wa Tanzania kujadiliana, Mwalimu akakubali heshima ya mkutano huo wa pekee ufanyike Tanganyika. Huo ulikuwa uamuzi wenye busara kwa kuwa wakati huo katika ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika, Tanganyika tayari ilikuwa nchi huru na mapambano dhidi ya ubeberu na ukoloni mkongwe yalikuwa yamepamba moto.

Mwenyekiti wa mkutano alikuwa Bibi Titi Mohamed wa Tanganyika na Katibu Mkuu alikuwa Madam Jean Martin Cisse kutoka Guinea. Mratibu kutoka serikali huru alikuwa Diallo Telli wa Guinea ambaye baadaye alikuwa Katibu Mkuu wa kwanza wa OAU.

Mama Maria Nyerere na Mwalimu walikuwa wenyeji wa mkutano wakisaidiwa na Rashidi Kawawa wakati huo Kaimu Waziri Mkuu na mkewe Sofia Kawawa

Waasisi walipania kukaza mikaja na kuwa bega kwa bega na wanaume wakati wote wa mapambano hadi ushindi kamili ili washirikiane katika kufaidi matunda ya Uhuru.

Katika kilele cha mkutano huo, wanawake walitoa azimio la kuunda PAWO ambayo ilizinduliwa mwaka 1974 na kuwa tapo la kuchochea vuguvugu la ukombozi na umoja wa Afrika katika nyanja zote. Wanawake wa Kiafrika walitambua wana haki ya kushiriki katika ngazi zote za kupanga sera na kutoa uamuzi na si kupokea maagizo tu.

Tanzania imeshuhudia wanawake walivyoimarisha umoja wao wakiongozwa na Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT). Mathalan, Julai 31, 1966 UWT iliandaa maandamano hadi Ikulu wakiongozwa na mwenyekiti wao, Bibi Titi Mohamed na kupokewa na Nyerere, aliyekuwa Rais wa Kwanza wa Tanzania.

Wanawake walimkumbusha Rais i wapi ile ahadi iliyowekwa na TANU na ASP wakati wa kupigania uhuru kuhusu haki na usawa kwa wake, waume na watoto katika maeneo mbalimbali hususan nafasi sawa za kazi serikalini.

Nia ya Tanzania kuleta haki na usawa iko kwenye nembo ya taifa. Katika nembo hiyo, kuna mwanamke na mwanamume na katika ubeti wa kwanza wa wimbo wa taifa, unaanza na Mungu ibariki Afrika kuthibitisha nia ya dhati ya kuwa na taifa moja lenye nguvu. Si hivyo tu wimbo wa taifa unaweka mkazo kwamba "wake kwa waume na watoto hizi ni ngao zetu" ikiwa ni ishara kwamba tunataka maendeleo yenye dhamira mujarabu.

Kuhusu vita vya ukombozi wa Afrika, wanawake katika nchi zilizokuwa mstari wa mbele katika mapambano, walifanya kazi kwa bidii katika uzalishaji wa chakula, mavazi, kulea watoto wa wapiganaji kwenye vituo, kuhudumia wagonjwa na majeruhi wa vita na kutoa ushauri nasaha kwa walioathirika kisaikolojia kwa madhila na madhara yaliyosababishwa na vita na kuishi kama wakimbizi.

Wapiganaji wengi walishuhudia wenzao wakilipuliwa na mabomu ya wakoloni na kuona miili yao ikikatwa na kutawanyikia porini. Waliotoa huduma za kwanza kwa majeruhi hao ni wanawake; walipwapa moyo manusura kwamba wamejitoa mhanga ili vizazi vijavyo viishi kwa amani.Wanawake waliwabeba vijana hao hadi kambini na wengine kuwazika huko porini. Mpaka leo, marehemu hao hawajapumzika kwa amani kwa sababu Afrika bado haijawa huru. Sasa Waafrika wanapigana wenyewe kwa wenyewe! Wanajiuliza jamani madhila haya yataisha lini? Wanawake na watoto wataangalia hii hali na kunyamaza mpaka lini wakati bara letu linajimaliza?

Wanawake walifanya kazi za hatari kama kusafirisha shehena za vyakula na silaha msituni kwa wapiganaji. Kadhalika wanawake walikuwa na majukumu mazito ya ukachero na kukusanya taarifa muhimu za kiusalama zilizosaidia kujua adui wako wapi na wanafanya nini.

Pia wanawake hawa wengi tunawakumbuka, tunawathamini, tunawashukuru japo wengi hawana majina wala makaburi yao hatuyajui, wengi ndoa zao zilivunjika na kuwaacha watoto yatima na wengine walifariki bila kuacha hata mtoto wa dawa.

Nchi nyingi zilipata uhuru wa bendera na baadhi kama Tanganyika na Zanzibar na waasisi wetu waliunda Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na kuanzisha mbio za kuwa na bara moja na serikali moja. Azimio la Arusha liliweka mikakati ya jinsi Tanzania itakavyojitawala kisiasa na kujitegemea kiuchumi ili kuleta haki, usawa na ustawi wa jamii.

Tumejifunza mengi katika miaka takriban 60 ya uhuru; ni wakati muhimu wakufanya tathmini ya wapi tunakwenda. Tukizingatia wosia wa waasisi wa PAWO na OAU kwamba ubeberu utaendelea kuwa hai hadi pale tutakapoamua kubadilisha fikra na vitendo vyetu.

Hiyo ni kama alivyosema Amilcar Cabral, kiongozi shujaa wa Guinea Bisau na Cape Verde aliyeuawa kikatili kwamba: "Hatuwezi kupambana na hili donda ndugu linaitwa ubeberu kama matumbo yana njaa na kichwani hakuna kitu... hata tuki husudu na kuvutiwa na maisha ya watu wengine haitusaidii; tunaweza kubadili maisha yetu kama tutakua na msingi imara wa kujitambua, juhudi zetu na kukubali kujitoa mhanga ili kizazi chetu kifaidike."

Japo tuliitemea mate mbingu na kuchafua nyuso zetu, kwa kuamini sera za kiliberali zingetusitiri, utabiri wa waasisi wetu umetimia kwamba baada ya ukombozi wa kisiasa, vita vikali vya ukombozi wa kiuchumi vitaendelea.

Safari hii si vita vya kumwaga damu bali ni vita vya kimkakati na diplomasia ya kudai haki bila kumwonea haya mtu. Kama waasisi wa PAWO waliweza kwenye vita vya ukombozi wa kisiasa na kushinda, je, kizazi hiki tumejipanga vipi kupambana? Tutapambana vipi na dhana potofu kwamba sisi Waafrika na hasa wanawake hatuwezi kungana na kujenga uchumi mkubwa na kuwa taifa kubwa duniani?

Je, wanawake wa Afrika tutashiriki vipi kuhakikisha kwamba waafrika wote popote pale walipo tunaweka bunduki zote chini na kuziteketeza ili tuwe na amani ya kudumu kujenga Afrika yetu Afrika huru? Ni wakati mwafaka sasa PAWO kama asasi maalum ya kuishauri AU kupendekeza kamati ya kuchagiza vita vya ukombozi wa kiuchumi iundwe.

Rais Samia Suluhu Hassan ameahidi atawaangalia wanawake wa kizazi hiki kama jeshi la ukombozi wa uchumi wa Afrika. Ni wajibu wetu kuchakarika na kuongeza juhudi chanya kwa umoja.

Tuchukue fursa hii sasa kwani bila uchumi thabiti na ustawi wa jamii bado hatutakuwa huru wala salama. Tusingoje kesho!

- **Imetayarishwa na Marie binti Shaba kwa ajili ya wanawake wa Afrika,**

# Chama ODM chajiondoa kwenye muungano NASA

**Nairobi,** KENYA

UPINZANI Kenya umeanza ukurasa mpya baada ya chama cha Orange Democratic Movement (ODM) kujiondoa kwenye muungano wa NASA muda mfupi baada ya vyama vikongwe vya WIPER na ANC kujitenga nao.

Hayo yanajiri wakati siasa za Kenya kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2022 zinazidi kushika kasi.

Muungano wa NASA unasambaratika, huku muungano mpya wa Okoa Kenya Alliance, ukikabiliwa na misukosuko kwa kuwa wadau watarajiwa bado hawajafikiana kuhusu mustakabali wao.

Chama tawala cha Jubilee, nacho kiko kwenye harakati za kumnadi kiongozi wa ODM Raila Odinga katika eneo la Mlima Kenya. Chama cha Orange Democratic Movement, kilitangaza kujiondoa rasmi kwenye muungano wa upinzani wa NASA ambao umekuwa ukilegalega.

Tofauti zilijiri baada ya mzozo wa kugawa ruzuku ya vyama vya kisiasa kuzuka.

Kwa sasa ODM inatishia kutowagawia wadau wa NASA ruzuku hiyo ya jumla ya Sh.milioni 153.

Kwenye kikao cha Baraza Kuu la ODM, wanachama wanawasihi wadau kubadili mitazamo yao.

Ifahamike kuwa ili muungano huo wa NASA ulioundwa 2017 usambaratike kisheria, sharti vyama vitatu vijondoe rasmi kwa kumtaarifu msajili wa vyama. Duru zinaeleza kuwa kiongozi wa Wiper iliyomeguka mapema wiki hii, Kalonzo Musyoka yuko kwenye harakati za kufanya mazungumzo ya kina, yatakayoamua hatima yao kisiasa.

Kiongozi wa ODM Raila Odinga sasa yuko kwenye jukwaa moja na mwenzake wa KANU Gideon Moi.

Chama cha KANU kinaegemea upande wa chama tawala cha Jubilee, hata hivyo viongozi wake wanashikilia kuwa hawajafikia mwafaka na yeyote kisiasa.

Nick Salat ni Katibu Mkuu wa KANU na analisisitizia hilo.

**VOA**



Wahamiaji wakiokolewa kutoka kwenye boti walilokuwa wakisafiria na kuingizwa ndani ya meli ya uokoaji ya Kijerumani katika operesheni iliyofanyika katika bahari ya Mediterranian pwani ya Lipya juzi. **PICHA: REUTERS**

# Wahudumu afya Wakenya waula nchini Uingereza

**Nairobi,** KENYA

KENYA imesaini makubaliano na Uingereza, ambayo yatawaruhusu wauguzi wake wasio na kazi na wahudumu wengine wa afya kufanya kazi Uingereza.

Waziri wa Afya wa Uingereza Sajid Javid na Waziri wa Kazi wa Kenya, Simon Chelugi, walitia saini makubaliano hayo hapo juzi, katika siku tatu ya ziara ya Rais Uhuru Kenyatta, London.

Mpango huo uko wazi kwa wafanyakazi wa afya wa Kenya, ambao wamehitimu na hawana kazi, kuhakikisha mchakato huo unaifaidisha Kenya, kulingana na taarifa kutoka kwa serikali ya Uingereza.

Mpango huo uliombwa na Kenya na unapaswa kuruhusu wataalamu na wasimamizi wa afya kufaidika na njia maalum kupitia mfumo wa uhamiaji wa Uingereza, kabla ya kurudi kazini katika sekta ya afya ya Kenya.

Maelezo kamili pia yanapaswa kuthibitishwa kabla ya mwisho wa Oktoba.

Chama cha Madaktari Kenya katika miaka ya hivi karibuni kimeibua wasiwasi kuhusu kiwango kikubwa cha ukosefu wa ajira kati ya madaktari na wauguzi nchini humo.

Makubaliano na Uingereza yanaweza kuwavutia wafanyakazi wengi wa huduma ya afya Kenya kwa kuwa wamekuwa wakilalamikia hali mbaya ya kufanya kazi, malipo duni na hata kufanya kazi kwa miezi bila malipo.

Hofu ni kwamba hatua hiyo inaweza kuwahamisha wafanyakazi wengi kutorokea Uingereza.

Hivi sasa kuna karibu Wakenya 900 wanaofanya kazi katika Huduma ya Kitaifa ya Afya ya Uingereza katika nafasi mbalimbali, kulingana na mamlaka za Uingereza.

Nchi hizo mbili pia zimezindua Muungano wa Afya wa Kenya na Uingereza, ambao utaongeza utafiti na ushirikiano kati ya Uingereza na vyuo vikuu vya Kenya na hospitali za mafunzo.

Ushirikiano wa kwanza utasaidia kuboresha matibabu ya saratani.

**BBC**

# China yaionya Uingereza baharini

**Beijing,** CHINA

CHINA imeionya Uingereza kuhusu kundi la meli zake za kivita zinazokaribia katika bahari ya Kusini mwa China dhidi ya vitendo vyovyote visivyofaa wakati inaingia katika eneo hilo linalozozaniwa.

Msafara wa meli hizo unaongozwa na meli ya kubeba ndege za kivita ya HMS Queen Elizabeth.

Jeshi la Wanamaji la Ukombozi wa Watu liko katika hali ya juu ya utayari wa mapigano, lilisema jarida la Global Times, linaloonekana kutumiwa kutoa kauli za Chama tawala cha Kikomunisti cha China (CCP).

China inapanua uwezo wake wa kinyuklia, wanasayansi.

China imekuwa ikifuatilia kwa karibu kinachofanyika katika safari ya msafara huo unaelekea upande wa mashariki kwenda Japan.

Nchi hiyo imeishtumu Uingereza kwa kuendelea kuishi katika siku zake za ukoloni.

Jeshi la Wanamaji la Uingereza limekuwa likifanya mazoezi na jeshi la wanamaji la Singapore na Katibu wa Ulinzi wa Uingereza Ben Wallace, ameonyesha wazi nia ya kuendelea kufanya mazoezi ya Uhuru wa kusafiri baharini kupitia Bahari ya Kusini mwa China.

Kinyume na uamuzi wa korti ya kimataifa ya 2016, China inadai sehemu kubwa ya bahari hiyo kuwa yake na imekuwa ikijishughulisha na kujenga visiwa bandia na njia za kuwezesha ndege kupaa zingine zikiwa karibu na maji ya eneo la nchi jirani.

Meli za kivita za Marekani na Uingereza zimepinga madai ya Uchina juu ya kumiliki Bahari ya Kusini mwa China kwa kuipitia katika bahari hiyo kwa makusudi.

**BBC**

# Muslim Brotherhood 24 kunyongwa nchini Misri

**Cairo,** MISRI

MAHAKAMA ya Misri, mwishoni mwa wiki imewahukumu kifo wafuasi 24 wa chama cha Muslim Brotherhood, kwa kuwaua maofisa wa polisi katika matukio mawili tofauti.

Mahakama ya uhalifu ya Damanhour, Kaskazini mwa mji mkuu Cairo, imelikuta kundi la watu hao na hatia kwa makosa kadhaa ya uhalifu, ikiwamo madai ya kushambulia kwa bomu basi lililokuwa linasafirisha maofisa wa polisi katika Mkoa wa pwani wa Beheira, mwaka 2015.

Shambulio hilo liliuwa maofisa watatu wa polisi na kujeruhi wengine wengi.

Washtakiwa wanane kati ya 24 walihukumiwa bila kuwapo.

Hukumu ya kifo kwa raia waliokutwa na hatia Misri, inatekelezwa kwa kunyongwa.

Hukumu hizo zinaweza kukatiwa rufaa, chanzo cha mahakama kimeongeza.

Misri ililipiga marufuku kundi hilo la kiislamu mwaka 2013, baada ya jeshi kumuondoa madarakani rais wa zamani Mohamed Morsi.

Tangu aongoze jeshi na kuwa rais, Abdel Fattah al Sisi alifanya msako mkali kwa chama cha Muslim Brotherhood na maelfu ya wafuasi wake walifungwa jela.

**VOA**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GEORGE MOHAMED MAGANGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya **GARI YENYE** jina la **BEN ES HAQ LTD** aina ya **IVECO** yenye namba za usajili **T 892 ALZ.**Chasis **No. QRZ112445,** Engine **NoQHZ093044** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/DOM/RB/372625/2021.**

### KUPOTEA KWA CHETI



**ROBERT HILARY** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo,cha kidato cha nne chenye index namba **S0547/0180** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **MAZWI** mwaka **2009,**na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S4071/0518** kilichotolewa na shule ya secondary ya **AGGREY CHANJI** mwaka **2012**,yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa OB/RB/1876/2016**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya ….KINONDONI**
**Kituo cha …..SINZA**
**Usimamizi wa mirathi na 199/2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU CAROLINE NGOMA SANDRO wa SINZA katika**
**SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA**
**NA GRACE ALEWANYO MUSHI**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo…..mwezi…mwaka…kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia.**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
**Imetolewa leo tarehe 26 mwezi 7 mwaka 2021.**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GEORGE MOHAMED MAGANGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya **GARI YENYE** jina la **BEN ES HAQ LTD** aina ya **IVECO** yenye namba za usajili **T 892 ALZ.**Chasis **No. QRZ112445,** Engine **NoQHZ093044** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/DOM/RB/372625/2021.**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BONIFACE NTOWANGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya **GARI** aina ya **TOYOTA NOAH** yenye namba za usajili **T 975 BQC.**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/DOM/RB/ 374317/2021.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**SHINYANGA**
**MAOMBI YA RUFAA NA. 48 YA 2020**
**(SHAURI LA MADAI NA. 16 YA 2013 KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA MASWA)**
**1. BUCHAMBI MISOBI…………MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**2. JILALA MAGASHI**
**(Msimamizi wa mirathi……………..MJIBU RUFAA ya marehemu SHABANI NYANDA)**
**Kwa: JILALA MUGASHI**

**TAARIFA YA KUITWA SHAURINI**

Hii ni kukupa taarifa kuwa, muombaji amefungua shauri la maombi tajwa hapo juu dhidi yako. Maombi hayo yamepangwa kusikilizwa tarehe **1/9/2021** saa **3:00 asubuhi** mbele ya **Mhe. Jaji G.J. Mdemu.** Hivyo unaamriwa kuhudhuria siku hiyo bila kukosa, na kama haukuhudhuria maombi hayo yatasikilizwa na kutolewa uamuzi bila wewe kuwepo.
Imetolewa kwa amri yangu na lakiri ya Mahakama hii leo **Tarehe 6/7/2021.**

R. M. MBUYA
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA YA SHINYANGA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA.**
**Usimamizi wa mirathi Na.32/2021.**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ANITHA GEORGE KIMAKO WA DODOMA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA AZIZA JUMA IDDI**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 18 mwezi 08 mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
**Imetolewa leo tarehe 30 mwezi 07 mwaka 2021.**

HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANI**
**KANDA YA MBEYA**
**SHAURI LA RUFAA JINAI NA. 69/ 2019**
**(Asilia Shauri la Jinai Na.2/2018,Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya)**
**JAMHURI……………………….MRUFANI**
**DHIDI YA**
**JOSEPH JUMA KYANDO…………………MJIBU RUFAA**
**KWA BWANA : JOSEPH JUMA KYANDO**
**POPOTE ULIPO…TANZANIA.**

**KUITWA SHAURINI**

Unaamuriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya Tarehe **27/08/2021** siku ya **Ijumaa saa 03.00** asubuhi bila kukosa.
**ELEWA KWAMBA**,Ukikosa kufika siku hiyo, Shauri litasikilizwa upande mmoja bila **WEWE** kuwepo na Uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii Tarehe 13 Mwezi July, 2021.

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**

### KUPOTEA KWA CHETI



**JUDITH AZAEL MAUKI** anatangaza kupotelewa na cheti cha chuo kozi ya **DIPLOMA IN EDUCATION MANAGEMENT AND ADMINISTRATION** chenye registration namba **0003410,** kilichotolewa na chuo cha **ADEM BAGAMOYO** mwaka **2017**,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**POLISI TAARIFA**
**DSM/PHQ/RB/220370/2021**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Bwana **SUBIRA ABUBAKAR KABYEMERA** amepotelewa na kadi ya gari namba **T440ATS.**Taarifa ya kupotea kwa kadi imefunguliwa katika kituo cha polisi Bukoba kwa jalada namba **KAG/BUK/RB/372711/2021.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi au awasiliane na mhusika kwa simu namba **0620409244**

### KUPOTEA KWA VYETI



**KENNEDY AJEX TEMU** anatangaza kupotelewa na vyeti,cha kidato cha nne chenye index namba S0938/0110 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya **MBEZI BEACH** mwaka 2006,na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0938/0719 shule ya **MBEZI BEACH** mwaka 2009,na cheti cha **CHUO KIKUU DODOMA kozi ya BACHELOR OF COMMERCE IN FINANCE(B.COM FINANCE)** registration namba **B.COM(FN)00001036 mwaka 2012.**

**POLISI TAARIFA:DAR/URA/RB/378281/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

### HATI YA KIAPO

Mimi **ATHUMANI SHAFII ANZUANI** mtu mzima mwenye akili timamu, mkazi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga, naapa kama ifuatavyo:-

1. Kwamba, Mimi **ATHUMANI SHAFII ANZUANI** ni Msimamizi wa Mirathi Na. 31/2021 ya Marehemu **MWALIM ANZUANI.**
2. Kwamba Marehemu **MWALIM ANZUANI** alikuwa ni mmiliki wa Nyumba Kitalu Na. 14 Block "38" Ngamiani Tamga.
3. Kwamba, Hati ya Umiliki wa Nyumba hiyo imepotea na nimetafuta pasipo matumaini ya kuipata tena.
4. Kwamba, kwa kiapo hiki naiomba Ofisi ya Ardhi Mipango Miji Tanga inipatie hati nyingine ya umiliki wa Nyumba Kitalu Na. 14 Block "38" Ngamiani Tanga kwa jina la **MWALUM ANZUANI.**

**UTHIBITISHO**
Mimi **ATHUMANI SHAFII ANZUANI** nathibitisha kuwa yote niliyoyasema hapo juu kuanzia aya ya 1 – 4 ni kweli tupu kwa jinsi nijuavyo na kwa mujibu wa sharia ya viapo (The Oaths and Statutory Declaration Act. Cap. 34 R:E 2019).
**Imethibishwa hapa Tanga**
Mbele ya ……………………………………….
Tarehe ………………………………………..
Answani …………………………………….
Cheo ………………………………………..
Sahihi …………………………………..

**Sahihi ya Muapaji**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**COSMAS MAPUNDA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA RAV 4 OLD MODEL yenye namba za usajili T 810 AGN chasis namba SXA110017050 engine namba 351916997,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa KW/RB/3691/2021**

### KUPOTEA KWA VYETI



**SPORA HENRY MALUGU** anatangaza kupotelewa na cheti che kidato cha nne chenye index namba **S.0617/0026** kilichotolewa na **LUSANGA SEKONDARI** mwaka **2008.** Vyeti vya **EBONITE TEACHERS COLLEGE (CERTIFICATE NA MATOKEO)** vya **EBONITE TECHERS COLLEGE** mwaka **2010.** Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. **Control No. 9910826628721.**

**MBEYA**
**KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA. 77 2019**
**(Asili Shauri la Hujuma Na.1/2018.Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya)**
**JAMHURI……………………MRUFANI**
**DHIDI YA**
**KENEDY LUPEMBE SIMSOKW…...……….MJIBU RUFAA NA.1**
**MATHEW ELIKANA MWANJALA…………MJIBU RUFAA NA.2**
**SHABAN MKWICHE……………………MJIBU RUFAA NA.3**
**KWA BWANA: 1. KENEDY LUPEMBE SIMSOKWE**
**2. MATHEW ELIKANA MWANJALA**
**3. SHABAN MKWICHE**
**POPOTE MLIPO-TANZANIA.**
**KUITWA SHAURINI**

Mnaarifiwa na Mahakama hii, kuhudhuria hapa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya Tarehe 27/09/2021 siku ya Jumanne saa 03.00 asubuhi bila kukosa, ambapo shauri limepangwa kusikilizwa.
ELEWENI KWAMBA,Ukikosa kufika siku hiyo, Shauri litasikilizwa upande mmoja bila WEWE kuwepo na Uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama hii leoTarehe 09 .07. 2021.

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

TOM alipooa alidhani kuwa ataishi kwa amani, furaha na kupata utulivu kama inavyokuwa kwa rafiki na wenzake wote waliofanya hivyo.
Siku zote ndoa ni masikilizano, maelewano, na anayeoa hupata furaha na heshima. Kinyume chake, kwake imekuwa ni misukosuko, mikosi na balaa. Badala ya kuwa ndoa yenye furaha, akajiingiza kwenye mtego hatari ambao hata baada ya kuufahamu, hakuweza kuutegua tena. Alichelewa. Ukawa ni mwanzo ni vilio, maafa na mtiririko wa mambo ya kushangaza.
Hebu pata kila nakala ya gazeti hili kufuatilia kisa hiki cha kushangaza na kusikitisha.

# Namsaka mke wangu-5

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

"Kwa nini ulichagua kazi hii na si nyingine?"

Kwanza Tedi alitaka kukasirika. Kwa sababu kazi anayoifanya inanasibishwa na uhuni wakati si kweli. Uhuni ni tabia ya mtu mwenyewe, hata akifanya kazi benki.

Baadaye alizimeza hasira zake na kujibu kwa akili.

"Nilishauriwa na rafiki yangu aliyenikaribisha nyumbani kwake. Na mimi nikuulize?" Tedi naye alimgeuzia kibao. Hii ni baada ya kumaliza kula.

"Niulize tu." Alisema huku akijilaza kitandani.

"Kwa nini umeniuliza maswali hayo?"

"Nimekuuliza kwa sababu wewe ni msichana mzuri sana. Si rahisi sana msichana kama wewe kufanya kazi kama ile. Kuna kitu gani unakitafuta au unakiwinda?"

Ni swali ambalo liligeuza hali ya hewa. Tedi aliangua kilio. Kilio kilichomshangaza Tom. Aliinua na kukaa kitandani. Alikilaza kichwa cha Tedi kwenye miguu yake na kumbembeleza.

"Samahani mpenzi kama nimekuudhi."


Zilipita dakika tano, ndipo Tedi alipoinua mdomo wake "Mpenzi hujafanya kosa kuniuliza swali hilo. Wala hakuna haja ya msamaha. Ila ni kwamba sijawahi kuulizwa swali hili na mtu yoyote. Sijawahi hata kupewa thamani hii ya kubembelezwa na wewe hapa. Kilio changu kimebeba machungu mengi sana. Ni kweli mimi siyo msichana na kuuza baa. Nafanya hivi kwa malengo tu, lakini kwa jinsi ilivyo sijui kama nitayafikia." Alisema na kuanza kulia tena.

"Usilie Tedi, hebu niambie. Inawezekana kabisa naweza kukusaidia."

Kwa mara ya kwanza Tedi alideka. Ameshapata mtu wa kumdekea. Wa kulala miguuni. Kifuani, na kulia huku akibembelezwa kama malkia. Pamoja na kulia, lakini alijihisi mtu mpya.

"Mimi hadi kufanya kazi hii nimepitia mengi sana. Nimeteseka sana kwenye maisha haya. Nimeteseka na watu baki, nimeteseka na ndugu zangu mwenyewe. Nitakuhadithia historia ya maisha yangu. Maisha machungu ambayo hutoamini kuwa ni mimi ndiyo nimeyapitia."

Wakati huo, Tom alikuwa akichezea nywele zake, kitu ambacho kilimpa raha sana Tedi.




**"Nilikwambia kuwa hata mimi ninaifanya kwa dhiki, lakini si kwa sababu naipenda. Kama umeamua niendelee kwa muda sawa, ila du nashukuru."**

Ni kama alikutana na binadamu anayejua utu. Anayejua thamani ya mwanamke. Anayejua kupenda na si kutamani au kuwa na uchu.

"Nilizaliwa Manyoni mkoani Singida. Baba yangu alifariki nikiwa na miaka sita. Ilibidi mama achukuliwe na mjomba. Nilikuwa na miaka 13 tu kila mwanaume alianza kuuona uzuri na urembo wangu. Mjomba wangu naye alikuwa miongozi mwao. Akaanza kunitongoza nikiwa bado nasoma. Nikakataa. Hapo visa vikaanza, anamfukuza mama yangu nyumbani kwake. Mama kisa alikuwa hajui, lakini nilikuja kumwambia baadaye." Alinyamaza na kumtazama Tom kwa wizi.

Tayari Tom alishaanza kuzama kwenye stori hiyo, hivyo alikuwa makini.

"Mama akaanza kuuza pombe za kienyeji ili kunitunza na kupata mahitaji mengine. Nilipoanza kidato cha kwanza tu, mama naye akafariki dunia." Machozi yalianza kumtoka.

"Pole sana Tedi. Hayo ndiyo maisha. Hakuna binadamu anayepitia maisha ya raha moja kwa moja. Ni lazima utapitia maisha magumu, tabu na dhiki, jikaze mama." Alibembeleza Tom.

"Hapo ndipo maisha yangu yalianza kuwa magumu. Nilichukuliwa na baba mdogo na kwenda kukaa kwake. Kwa sababu alikuwa na kiduka kidogo aliniweka ili niwe nauza bidhaa. Lakini mwisho wa siku naye alinitongoza. Kumbe yote yale mpango wake ulikuwa ni kutembea na mimi. Nikakataa. Akatengeneza stori kuwa mimi nalazimisha nitembee naye, mkewe akanifukuza. Nikajiona nina bahati mbaya sana duniani. Mjomba ilikuwa hivyo. Leo baba mdogo mambo ni hayo hayo. Nilichoka kabisa. Unajua kuchoka mpenzi." Bado Tedi alizidi kusimulia maisha yake huko nyuma.

"Sikufichi mpenzi, kutokana na ugumu wa maisha, niliingia kwenye mahusiano na wanaume wawili kwa nyakati tofauti, lakini kiukweli nilikuwa na malengo yangu. Kuna siku alikuja mama mmoja ambaye wakati wa usichana wake alikuwa anaishi kijiji kwetu Manyoni, akanitaka niondoke naye twende Dar es Salaam kuna kazi. Kumbe mama huyo alikuwa anamiliki danguro. Nilifanya kazi hiyo kwa lazima bila kupenda, tukawa tunafanyishwa kazi hiyo bila malipo. Pesa yote mama hiyo anachukua. Sisi ni nguo, kula na matibabu ambayo pia yalikuwa ni hafifu. Kuna siku mimi na rafiki yangu Nora tulitumwa sokoni tukatoroka na kuja hapa kwao Morogoro."

"Okay mpenzi, sasa kwa nini umeamua kuingia kwenye kazi hii wakati kuna kazi nyingi za kufanya?"

"Kumbuka tumefika hapa hatukuwa na chochote kile. Ilibidi mimi nikubali kufanya kazi hii, huku tukicheza mchezo. Lengo baada ya mwaka nipate pesa nikajifunze kazi ya urembo, kupamba na kusuka ili baadaye Mungu akijaalia nifungue saluni yangu."

"Una uhakika kuwa utafanikiwa kwa jinsi mambo yanavyokwenda?"

"Mhh, bado mambo magumu. Unajua mambo ni mengi. Matarajio ni mengi, lakini kipato ni kidogo baba." Tedi aliongea kwa unyonge.

Tom alimtazama Tedi kwa jicho la ndani kidogo hadi mwenyewe aligundua hilo.

"He, mbona umenitazama hivyo?" Alisema huku akitabasamu. Lilikuwa ni tabasamu halisi.

"Tedi?"

"Abee."

"Kwanza pole, sana kwa yote yaliyokukuta. Mimi pamoja na kwamba tumekuja tu hapa ili tuupitishe usiku wa leo, nimeguswa sana na historia ya maisha yako. Kwa hiyo mimi naamua kujitolea kukulipia ada ya kujifunza mambo ya urembo."

Tedi ni kama vile alikuwa kwenye ndoto. Moja ya ndoto chache alizowahi kuota maishani mwaka. Alibaki ameduwaa kama amepigwa ganzi.

"Ni suala la kwenda tu huko na kuuliza ada ni kiasi gani ili nikalipie benki. Halafu napenda niwe mmoja alio ndani ya mafanikio yako, hivyo utakapomaliza mafunzo, mimi nikajitolea kukununulia vifaa vyote vinavyohitajika kwenye saluni."

Ni muda ambao Tedi ni kama alirudiwa na akili ghafla. Akainuka kwenye miguu ya Tom ambayo alikuwa ameilalia. Akamkubatia kwa nguvu kifuani kana kwamba anataka kumkaba. hakutegemea kitu kama kile maishani.

"Hivi ni kweli mpenzi?"

"Siwezi kukudanganya."

"Sasa nifanye nini?"

"Kuhusu nini Tedi?"

"Unataka tena niendelee na kazi hii?"

"Mimi sipendi. Ila endelea kidogo kwa ajili ya kupata pesa za kujikimu, baadaye tutaangalia nini tufanye sasa?"

"Nilikwambia kuwa hata mimi ninaifanya kwa dhiki, lakini si kwa sababu naipenda. Kama umeamua niendelee kwa muda sawa, ila du nashukuru."

Tedi alianza kujihisi kuwa ameanza kuwa mtu mwenye bahati. Maombi yake aliyokuwa akiomba tangu kufariki mama yake na kuishi peke yake akiwa na umri mdogo, anaona Mungu ameanza kumsikia mja wake baada ya miaka mingi.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**



# CARVAJAL
## asaini mkataba mpya Madrid

**MADRID, Hispania**

BEKI wa kulia wa Real Madrid, Dani Carvajal, ametia saini mkataba mpya utakaomweka katika klabu hiyo hadi 2025, timu hiyo ya LaLiga imesema.

Msimu wa 2020-21 wa Carvajal ulikumbwa wa majeraha, huku beki huyo mwenye umri wa miaka 29 akicheza mechi 15 katika mashindano yote ambapo Real Madrid ilimaliza LaLiga ikiwa nafasi ya pili mbele ya bingwa Athletico Madrid.

Hata hivyo, Real Madrid iliondolewa na Chelsea kwenye hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Carvajal amekuwa Madrid tangu 2013 na amesaidia timu hiyo kushinda mataji 16 yakiwamo manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, mawili ya LaLiga pamoja na Copa Del Rey.

Anaungana na kiungo Luka Modric, winga Lucas Vazquez na beki Nacho Fernandez katika kutia saini mikataba mipya Real Madrid kabla ya msimu wa 2021-22.

Real Madrid itaanza kampeni yake mpya ya LaLiga chini ya kocha mpya, Carlo Ancelotti kwa kucheza ugenini dhidi ya Alaves Agosti 14, mwaka huu.

## JUVENTUS WARUDI UPYA KWA LOCATELLI

**TURIN, Italia**

JUVENTUS imeamua kujitosa mazima katika mbio za kuwania kumsajili kiungo wa kimataifa wa Italia, Manuel Locatelli.

Kwa mujibu wa Goal.com Juventus imethibitisha kuanza mazungumzo mapya na Sassuolo kwaajili ya kumsajili Locatelli tayari kwa msimu mpya wa Ligi Kuu Italia.

Locatelli amekuwa mchezaji anayenyatiwa zaidi na Juventus baada ya msimu bora wa 2020-21 huko Sassuolo, pamoja na kuisaidia Italia kutwaa Kombe la michuano ya Euro 2020.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 pia amehusishwa na Arsenal, lakini anataka kuhamia kule Bianconeri na kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Juventus walikataliwa ofa ya mkopo ya miaka miwili na chaguo la kumnunua mchezaji huyo moja kwa moja kwa euro milioni 30.

Goal inataarifu kuwa Sassuolo wanataka angalau euro milioni 40 kwa kiungo huyo, ambaye yuko chini ya mkataba hadi mwaka 2023.




# Chiellini athibitisha kubaki Juventus

**TURIN, Italia**

MLINZI Giorgio Chiellini anajipanga kusalia katika Serie A na Juventus, yupo tayari kusaini mkataba mpya na klabu hiyo yenye maskani yake Turin baada ya mkataba wake kumalizika tangu Juni 30, mwaka huu.

Nahodha huyo wa Italia ametupilia mbali mashaka yanayodumu juu ya siku zake za usoni, akiwatuliza mashabiki kwa kusema atariposti kwenye mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya wiki ijayo.

"Nitakuwa Turin Jumatatu, kwani Massimiliano Allegri atakuwa ananisubiri huko," mlinzi huyo wa kati alisema.

"Nitakuwepo hata ikiwa ingekuwa vizuri kuwa na likizo. Nitajaribu kumaliza kazi yangu kwa kushinda mataji zaidi kwa sababu kushinda mataji kunanifanya niwe na njaa zaidi."

Chiellini alijiunga na Juventus mwaka 2005 na tayari amecheza mechi 535 kwa klabu hiyo. Mkataba wake mpya unatarajiwa kuongeza miaka miwili.

## HABARI MICHEZO

# POGBA

## PSG WAFANYA MAZUNGUMZO



**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Paris Saint-Germain -PSG imeripotiwa kuwasiliana na wawakilishi wa Paul Pogba ili kujua nia yake na uwezekano wa kuhamia kule Parc des Princes.

Mkataba wa sasa wa kiungo huyo wa Manchester United umebakiwa na miezi 12, na inaaminika alikataa kusaini mkataba mpya hapo Old Trafford.

Marcus Rashford ametajwa kujaribu kumshawishi Pogba kubaki United, lakini klabu hiyo inakuwa chini ya shinikizo la kumuuza msimu huu wa joto ikiwa atashikilia msimamo wa kutoongeza mkataba wake kusalia Old Trafford.

Kwa mujibu wa The Athletic, PSG sasa wamewasiliana na Pogba juu ya kuhamia Ligue 1, lakini miamba hao wa Ufaransa bado wanaweza kusubiri na kujaribu kumsajili kwa uhamisho wa bure mnamo 2022.

Ripoti hiyo inaongeza kikosi hicho cha kocha, Mauricio Pochettino, hakijawasiliana na United na ofa rasmi bado haijawekwa mezani, lakini Mashetani Wekundu hao wanajiandaa kwa lolote wiki zijazo.

Pogba amekuwa na mchango wa moja kwa moja katika mabao 80 kwa mechi 206 tangu aliporejea kwa mara ya pili hapo United na kocha Ole Gunnar Solskjaer bado ana matumaini kuwa klabu inaweza kumbakiza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28.

## LUKAKU KUIKAMUA MAMILIONI CHELSEA

**LONDON, England**

KLABU ya Chelsea imeripotiwa kujiandaa kuwajaribu Inter Milan kwa dau kubwa la pauni milioni 110 kuipata saini ya Romelu Lukaku.

Licha ya kutumia fedha nyingi kupata saini za Timo Werner na Kai Havertz katika msimu wa joto wa 2020, Chelsea inadhaniwa inataka kuongeza maboresho katika safu yake ya kati kwa msimu ujao.

Erling Braut Haaland wa Borussia Dortmund ndiye aliyetajwa kwa muda sasa kama lengo kuu la The Blues hao, lakini Chelsea inakumbana na changamoto la suala la bei iliyokadiriwa kuwa pauni milioni 149.

Lukaku amethibitisha mara kadhaa kwamba hafikirii kuondoka Inter, lakini kwa mujibu wa vyanzo vya Italia, Chelsea wapo tayari kujaribu kuwashawishi Inter kwa zabuni ya pauni milioni 110.

Ripoti zinabainisha kuwa bado hakuna ofa ilizopokelewa kwa Inter, lakini kutokana na hali ya kifedha ya klabu inawezekana wakashawishika kumwachia Lukaku, ambaye alifunga mabao 24 na kutoa asisti 10 Serie A msimu uliopita.



## SEVILLA YATANGAZA THAMANI YA KOUNDE

**SEVILLE, Hispania**


KLABU ya Sevilla inataka dau la karibu euro milioni 80 ikiwa makubaliano yatafikiwa na Chelsea ambayo inataka kumsajili nyota wake, Jules Kounde kuondoka pale kwenye dimba la Ramon Sanchez Pizjuan.

Kwa mujibu wa Goal.com Chelsea imeingia katika mazungumzo na beki huyo wa kimataifa wa Ufaransa na klabu ya Sevilla.

Kounde yuko wazi kwa wazo la kutafuta changamoto mpya katika Ligi Kuu England, lakini uhamisho utaruhusiwa endapo klabu hizo mbili zitakubaliana katika biashara hiyo.

Klabu kadhaa zilikuwa zinafuatilia mwenendo wa mchezaji huyo msimu huu wa joto ikiwamo Real Madrid, Manchester United na Chelsea lakini mpaka sasa bado hakuna timu iliyoweza kuwashawishi Sevilla kumwachia.

Klabu ya Manchester United wamejitoa kinyang'anyiro hicho baada ya kukamilisha usajili wa Rafael Varane kutoka Real Madrid, huku Los Blancos wakikosa fedha ya kufanya usajili mkubwa katika dirisha hili.



TANGAZO

## KWA UFUPI

**VILLA KUMZUIA GREALISH**
ASTON Villa wanatarajiwa kuanza tena mazungumzo na kiungo wa England, Jack Grealish mwenye umri wa miaka 25, wiki ijayo na wako tayari kumpa mkataba mpya wa kuzuia nia ya Manchester City kumsajili. ***(Express na Star)***

**CITY, VILLA WATETA**
BINGWA wa Ligi Kuu England, Manchester City, wameanza mazungumzo na Aston Villa kwa ajili ya kumsajili Jack Grealish mwenye umri wa miaka 25. ***(Guardian)***

**GUARDIOLA NA GREALISH**
KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, anatarajia kufanikisha usajili wa Jack Grealish kwa wakati kabla ya mechi za Ngao ya Jamii ambayo inatarajiwa kuchezwa ifikapo Agosti 7, mwaka huu. ***(Star)***

**LUKAKU: SIONDOKI**
MSHAMBULIAJI wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 28, ameweka wazi kuwa ana nia ya kubakia kwa mabingwa wa Italia, Inter Milan baada ya kukataa ofa ya kurudi Chelsea. ***(Gazzetta dello Sport)***

**POGBA KUTUA LIVERPOOL**
WAKALA wa Paul Pogba, Mino Raiola amemkabidhi kiungo huyo wa kati wa Manchester United na Ufaransa mwenye umri wa miaka 28 kwa Liverpool. ***(Le 10 Sport)***

**ZOUMA ANUKIA WEST**
KLABU ya West Ham wanaandaa dau la pauni milioni 20 kwa Kurt Zouma mwenye umri wa miaka 26 kwa ajili ya kumsajili kutoka Chelsea. ***(Mail)***

**ANDERSON KIMEELEWEKA**
GOLIKIPA wa Manchester City mwenye umri wa miaka 27, Ederson anatarajiwa kuongezewa mkataba mpya wa miaka mitatu. ***(Athletic)***

**WENGER ATAJWA USWISI**
KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger amehusishwa na nafasi iliyo wazi ya kocha wa Uswisi. Mfaransa huyo hajafanya kazi katika usimamizi wa soka tangu aondoke Arsenal alikokaa kwa miaka 22. ***(Blick, via Mail)***

**DEST KUBAKIA BARCA**
MLINZI wa Timu ya Taifa ya Marekani, Sergino Dest mwenye umri wa miaka 20, ameamua kubaki Barcelona na amekataa uhamisho wa kwenda klabu za Arsenal, Bayern Munich na Borussia Dortmund. ***(ESPN)***

**LOCATELLI SOKONI**
OFISA Mtendaji Mkuu wa Sassuolo, Giovanni Carnevali, amesema watakubali tu kumuuza kiungo wa kati wa Italia mwenye umri wa miaka 23, Manuel Locatelli, ambaye amehusishwa na uhamisho wa kwenda Arsenal na Juventus, ikiwa ofa mwafaka itatolewa mapema kabla ya kufungwa kwa dirisha la uhamisho. ***(Gazzetta dello Sport, via Mirror)***

**TRIPPIER AFUNGUKA**
MLINZI wa Atletico Madrid na England, Kieran Trippier mwenye umri wa miaka 30, anatarajia uhamisho wake kwenda Manchester United utachukua hadi mwisho wa dirisha la uhamisho. ***(Manchester Evening News)***

**WILLIAN KUUZWA**
ARSENAL iko tayari kusikiliza ofa kwa winga wa Brazil mwenye umri wa miaka 32, Willian wanapojaribu kupunguza kiasi cha fedha wanazotoa kama mishahara kwa wachezaji wao. ***(Star)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ARSENAL YAJITOSA KUMWANIA MARTINEZ

**Iko tayari kumtoa Bellerin ili kufanikisha mchakato wa kumnasa mshambuliaji...**

**LONDON, ENGLAND**

KLABU ya Arsenal ipo kwenye hesabu za kuinasa saini ya mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez ili kuwa ndani ya kikosi hicho kwa msimu ujao, kwa mujibu wa Football Insider.

Dau la kumpata nyota huyo ambaye bado ana mkataba ndani ya timu yake linatajwa kuwa ni pauni milioni 77.

Katika orodha ya washambuliaji ambao wanahitajika ndani ya Arsenal yupo pia Tammy Abraham ambaye anakipiga ndani ya Chelsea kwa sasa na thamani yake inatajwa kuwa pauni milioni 40.

Sababu kubwa ya mshambuliaji huyo kuwekwa kwenye hesabu na Arsenal ni uhitaji wa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mikel Arteta ambaye anataka kuipata saini ya raia huyo wa Argentina ambaye mkataba wake ndani ya Inter Milan umebakiwa na miaka miwili.

Kwa mujibu wa ripoti ya Football Insider, Arsenal wako tayari kumtoa beki Hector Bellerin kama sehemu ya mpango wao wa kumsajili, Martinez kutoka Inter Milan.

Arsenal hawawezi kufikia dau ambalo klabu ya Inter Milan inalihitaji kwa Martinez, lakini wanaamini kumtoa Bellerin kunaweza kupunguza gharama wanazotakiwa kulipa.

Bellerin anaweza kuelekea Inter Milan kama mbadala wa Achraf Hakimi, na klabu hiyo inahitaji fedha katika msimu huu wa kiangazi.

Bellerin amekuwa akikosa kuanza katika kikosi cha washikabunduki hao tangu Arteta alipochukua nafasi ya kukinoa kikosi hicho akitokea katika klabu ya Manchester

HABARI MICHEZO

# POLISI TANZANIA FC, BABA YAKE MDAMU WAFUNGUKA

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Polisi Tanzania umekanusha taarifa za kumtelekeza mshambuliaji wake, Gerald Mdamu ambaye alivunjika miguu katika ajali wakiwa wanatoka mazoezini wakati wanajiandaa na mechi za lala salama za kumalizia msimu wa Ligi Kuu Bara uliopita.

Taarifa za kutekelezwa mchezaji huyo zilipelekea wadau wa michezo kukusanya michango kwa ajili ya kusaidia matibabu ya mshambuliaji huyo.

Mdamu yuko katika hatari ya kukatwa mguu baada ya kudaiwa klabu yake imeshindwa kumpatia matitabu sahihi ambayo yangemfanya arejee katika hali yake ya kawaida.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Makamu Mwenyekiti wa Polisi Tanzania, Robert Munisi, alisema uongozi wa timu hiyo haujashindwa kumhudumia mchezaji wao kama ambavyo taarifa zimesambaa katika vyombo mbalimbali hapa nchini.

Munisi alisema mbali na Mdamu kuwa mchezaji wao, lakini Polisi Tanzania inamhesabu mchezaji huyo ni sawa na mtoto wao kutokana na baba mzazi wa nyota huyo kuwa mstaafu wa Jeshi la Polisi.

Munisi alisema klabu hiyo kamwe haiwezi kumtelekeza mchezaji wake na imekuwa karibu naye tangu alipopata ajali, akiwa na wachezaji wenzake.

"Gerald alipata ajali akiwa na basi la timu wakiwamo wachezaji wengine, ila mshambuliaji huyo ndio aliyeumia sana, sio ukweli kuhusu kukatwa mguu na matibabu yanaendelea vizuri,".

"Hatuna shida na familia ya Mdamu kwa sababu tumekuwa na mawasiliano mazuri na baba mzazi wa mchezaji huyo. Kitendo cha kutoka KCMC hadi Muhimbili, walivyofika hakupata matibabu kwa sababu alikutwa na shida nyingine ya figo, hivyo hakufanyiwa kipimo cha MRI," alisema Munisi.

Alisema hali hiyo ndio ilizua sintofahamu na kuzua taharuki na hakupata matibabu haraka kama ilivyotarajiwa kutokana na tatizo jipya la figo lilivyojulikana baada ya kuhofia kumwingiza kwenye mionzi.

"Polisi Tanzania hatujashindwa kumtibia mchezaji wetu huyo na kama ikishindikana kutibiwa hapa tuna uwezo wa kumpeleka nje ya nchi kwa ajili ya kutibiwa," alisema Munisi.

Baba mzazi wa nyota huyo, Mathias Mdamu alisema anasikitishwa na taarifa hizo kwa sababu amekuwa karibu na viongozi wa timu hiyo kuanzia ajali ilivyotokea hadi alipoomba mtoto wake ahamishiwe katika hospitali ya Muhimbili.

"Nashirikiana vizuri na uongozi wa Polisi kwa kila hatua, nasikitishwa na habari za Gerald kukatwa mguu ambazo sio za kweli, anaendelea vizuri," alisema baba huyo.



Mkurugenzi wa Mashindano wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF), Salum Madadi (kushoto), akimkabidhi golikipa wa timu ya vijana ya umri chini ya miaka 17 ya JKT Tanzania, Abubakari Manga, tuzo ya Kipa Bora wa Ligi ya Vijana 2021 iliyomalizika jijini Dar es Salaam juzi. JKT Tanzania walitwaa ubingwa huo. **PICHA: TFF**

# Nyota wapya ruhusa Kagame Cup

**Na Adam Fungamwango**

KLABU zinazoshiriki mashindano ya Kombe la Kagame zimeruhusiwa kutumia wachezaji wapya ambao wana mpango wa kuwasajili kwa ajili ya kuwatumia katika mashindano mbalimbali kwenye msimu ujao wa 2021/22.

Mkurugenzi wa Mashindano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Salum Madadi, alisema kanuni zinawapa nafasi timu zote kujumuisha wachezaji wapya ili kuboresha na kuongeza ladha katika michuano hiyo.

"Maandalizi yanakwenda vizuri. Tumeshafanya kila kitu, ikiwamo kuandaa hoteli na kila kitu. Kuhusu wachezaji, kanuni inatoa nafasi ya maingizo mapya kwa timu ambazo zitakuwa tayari. Hii ni kwa ajili ya kuleta ladha na kuboresha mashindano hayo," alisema Madadi.

Kauli hiyo ni faraja kwa timu za Tanzania ambazo zimeanza usajili kwa ajili ya msimu ujao na zimethibitisha kushiriki michuano hiyo.

Tayari Azam FC imeshatangaza kusajili wachezaji wapya ambao ni Rodgers Kola kutoka Zanaco, Charles Zulu (Cape Town City- Afrika Kusini), Paul Katema (Red Arrows), Kenneth Muguna wa Gor Mahia ya Kenya na Mtanzania, Edward Charles kutoka Ruvu Shooting.

Jumla ya timu nane zinatarajiwa kupambana kuwania taji hilo ambapo Kundi A linaundwa na wenyeji Yanga, Nyasa Big Bullet (Malawi), Atlabara (Sudan Kusini) na Express ya Uganda huku Kundi B likiwa na KCCA ya Uganda, Le Messager Ngozi (Burundi), KMKM (Zanzibar) na Azam FC.

# Biashara kusajili 'majembe' mapya

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA kuhakikisha kikosi chake kinakuwa imara na chenye ushindani, mabosi wa Biashara United wamesema wanatarajia kusajili wachezaji wengine wenye viwango vya juu ambao wataisaidia timu hiyo kufanya vyema katika Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa watakayoshiriki.

Katibu Mkuu wa Biashara United, Haji Mtete, aliliambia gazeti hili katika kuhakikisha wanatumia muda vyema, kikosi chao kimeshaanza mazoezi ili kuwaweka vizuri wachezaji wao.

Mtete alisema lengo ya kuanza mazoezi mapema ni kuwaweka tayari nyota wao kukabiliana na ushindani, huku viongozi wakiendelea na mchakato wa kusaka wachezaji wapya nane watakaokuja kukiongezea nguvu kikosi chao.

Kiongozi huyo alisema wanatarajia kusajili wachezaji wa nafasi mbalimbali na klabu hiyo ina uwezo wa kunasa nyota itakayemhitaji kutoka ndani na nje ya Tanzania.

**"Kuna watu hawa jui kwamba sisi tuna uwezo wa kusajili wachezaji kutoka nje ya nchi, na kwa uthibitisho tunao wachezaji kutoka Ghana, Kenya na Uganda ambao wamecheza Ligi Kuu ili omalizika, haitakuwa ajabu au mara ya kwanza kusajili wachezaji kutoka nje ya nchi," alisema Mtete.**

Biashara United ya Musoma mkoani Mara itashiriki michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa mara ya kwanza baada ya msimu uliokwisha wa Ligi Kuu Tanzania Bara kumaliza katika nafasi ya nne.

Michezo

Jumamosi Julai 31, 2021

Nipashe



# Arsenal yajitosa kumwania Martinez

HABARI UK. 22




Mwekezaji wa Simba, Mohammed Dewji 'Mo', akikabidhi hundi ya mfano ya Sh. bilioni 20 kwa Mwenyekiti wa klabu hiyo, Murtaza Mangungu (wa pili kushoto) na Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini, Adam Mgoyi (kulia). Kushoto ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, Ramadhan Kailima. **PICHA: SAADA AKIDA**

## Tanzania bingwa CECAFA

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Soka ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 23 (U-23), imefanikiwa kutwaa ubingwa wa mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) baada ya kuifunga Burundi penalti 6-5 katika mechi ya fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Bahir Dar nchini Ethiopia jana.

Timu hizo zililazimika kwenda hatua ya matuta baada ya kumaliza dakika 90 wakiwa sare ya bila kufungana, zikicheza mbele ya Rais wa CECAFA na Shirikisho la Soka Nchini (TFF), Wallace Karia.

Tanzania iliweka ndani ya penalti zote sita kupitia kwa Sospeter Bajala, Israel Mwenda, Lusajo Mwaikenda, Abdulrahman Mohamed, Lucas Kikoti na Rajab Athumani huku waliofunga kwa upande wa Burundi ni Issa Hazikimana, Erick Mgirizi, Juma Mohamed, Frank Ndiwimana na Ismail Nshirimana.

Wachezaji walioanza kwenye mechi hiyo ni Matacha Mnata, Nickson Kibabage, Lusajo Maikenda, Sospeter Bajana, Meshack Abraham, Reliants Lusajo, Kelvin Nashon, Abdulrazack Mohamed, Yusuph Mhilu, Andrew Senchimba na Israel Mwenda.

Tanzania ambayo ilitoka kwenye Kundi A, ilianza mechi zake Julai 21 ilipoichapa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo bao 1-0, kabla ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Uganda Julai 24, na kufanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali.

Kikosi hicho cha Tanzania kilichokuwa kinanolewa na Kocha Mkuu, Kim Poulsen kwa kushirikiana na Shadrack Nsajingwa kilitinga fainali baada ya kuichapa Sudani Kusini bao 1-0 katika mchezo wa nusu fainali.

# DEWJI ATIMIZA AHADI YAKE

## Aipatia Simba Sh. bilioni 20 na kusema ataongeza fedha nyingine endapo...

**Na Saada Akida**

AMETIMIZA! Mwekezaji na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Mohammed Dewji 'Mo', amekata mzizi wa fitna kwa kuweka kiasi cha Sh. bilioni 20 katika klabu hiyo baada ya kupata ridhaa kutoka kwenye Tume Huru ya Ushindani (FCC).

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Dewji alisema amefikia kutekeleza ahadi hiyo baada ya mchakato wa mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji kufikia asilimia 97 na yeye kupewa ridhaa na mamlaka husika ikiwamo FCC.

Dewji alisema kiasi hicho cha fedha alichoweka kitamwezesha kumiliki hisa za Simba kwa asilimia 49 huku kiasi kingine kilichobakia cha asilimia 51 kimebakia kwa wanachama wa klabu hiyo.

"FCC imeturuhusu kuingia hizo fedha, tayari Sh. bilioni 20 nimeingiza katika akaunti ya Simba SC Limited Company, mchakato haukuwa rahisi hadi kukamilika kulikuwa na maneno mengi sana kuhusu suala hili, ila sasa nina imani mjadala wa bilioni 20 nimelifunga leo," alisema Dewji.

Mfanyabiashara huyo alisema ana imani kitendo cha kuweka fedha hizo kitawafunga 'mdomo' wale ambao walidai hana fedha hizo za kuwekeza katika klabu hiyo ya Wekundu wa Msimbazi kama alivyoahidi mbele ya wanachama.

"Tangu tumeingia katika mchakato huu kuna mengi yaliyoongelewa ila watambue kwamba kwa miaka minne ya mchakato huu tayari nimeshatumia Sh. bilioni 21.3 ikiwamo usajili wa wachezaji, makocha na mambo muhimu kuhusu timu, hizi fedha zilizotumika ni fedha za ziada kulingana na mapenzi yangu na Simba , nina imani baada ya kuweka fedha hizo sasa tutajipanga kwa ajili ya mipango ya klabu," alisema Dewji.

Aliongeza ana imani Simba itatawala soka la Afrika na ni lazima uwepo uwekezaji kwa sababu bila fedha timu haiwezi kushindana na timu kubwa za Afrika ikiwemo Al Ahly ya Misri na nyingine.

"Simba ni taasisi kubwa na inaendeshwa kwa uwazi na nidhamu ya hali ya juu, hakuna mkubwa ndani ya klabu hii, hata mimi (Dewji), ni mdogo sana mbele ya Simba, kila kitu kinaenda kwa weledi mkubwa."

"Baada ya kuweka Sh. bilioni 20, Simba ina mipango mikubwa sana ikiwamo kujenga viwanja vinne mbali na ule Uwanja wa Bunju, maboresho ya timu ya vijana na timu ya wanawake ambayo nao wanakwenda kutuwakilisha katika michuano ya kimataifa," alisema Dewji.

Aliongeza Simba haitakubali kupokea mdhamini ambaye atatoa fungu sawa na timu zingine, kwa sababu thamani ya Simba kwa sasa imeongezeka na mchango wake umesaidia kuitoa katika nafasi ya 22 hadi 12, na kuifanya Tanzania iwakilishwe na timu nne kwenye mashindano ya kimataifa msimu ujao.

"Sikubali mdhamini aje kwangu kutoa sawa na timu zingine, tutatafuta mianya mingine ya kutafuta fedha, ikishindikana basi nitatoa mwenyewe kuongeza mzigo na klabu hii itajiendesha na kufikia malengo," alisema Dewji.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini, Adam Mgoyi, alisema mchakato wa mabadiliko unakaribia kufikia mwisho na tayari uko katika asilimia 97 huku akiweka wazi mambo machache ndiyo yamebakia ikiwamo uhakiki wa wanachama, mali na madeni ya klabu.

Naye Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu alisema wanatarajia kukutana na wanachama ili kuwaeleza masharti waliyopewa na FCC.

"Tutawaeleza wanachama masharti ambayo yameelezwa na FCC, ni haki yao katika uwekezaji huo, mbali na suala la kiasi cha fedha zilizowekwa na mwekezaji huyo," alisema Mangungu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002